

Mbona Unalialia? Nena!

Jeffersonville, Indiana, USA

Julai 14, 1963A

1 Bwana awabariki! Hebu na tuendeleo tu kusimama kwa muda, tunapoinamisha vichwa vyetu. Kuna haja maalum? Kama ungeweza, hebu ijulikane unapomwinulia Mungu mikono yako na kusema, kwa jambo hilo, "Bwana, unajua haja yangu."

2 Baba uliye Mbinguni, sisi ni watu tulioheshimika kabisa asubuhi hii kukutanika katika nyumba ya Mungu, tunapojua ya kwamba kuna watu wengi sana ambao wangetaka kuwa katika nyumba ya Mungu asubuhi ya leo na wamo hospitalini na vitandani mwa magonjwa. Nawe umetupa majaliwa haya ya kuwa hapa nje leo. Nasi hatuji kamwe, Bwana, kuonana mmoja kwa mwingine, ingawa tunapenda ushirika wa sisi kwa sisi, bali tungalifanya hivyo manyumbani mwetu. Lakini tumekuja hapa kushiriki na Yeye ambaye ametuleta pamoja kama watoto wapendwa na ndugu.

Tunakushukuru sasa. Na njia pekee tunayojua kushirikiana kwa usahihi na Wewe ni kuzunguka Neno Lako. Neno Lako ni Kweli. Tunakusanyika hapa kwa ajili ya nguvu za kiroho. Tunazihitaji, Bwana. Lazima tuwe na nguvu za kustahimili misalaba tunayobeba. Nasi tunaomba ya kwamba utamtuma Roho Mtakatifu mkuu leo, na atatuimarisha sisi sote. Tujalie mahitaji ya watu Wako wanapokutanika na kuinua mikono yao Kwako ya kwamba wanahitaji mambo kama hayo. Jibu kila mmoja, Bwana.

3 Tunakushukuru kwa kuyaokoa maisha ya Dada yetu Ungren jana usiku, katika ajali barabarani hapa juu. Wewe ulikuwa mwenye neema kwao, Bwana, nasi tunakushukuru kwa ajili ya jambo hilo. Na sasa tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utaendelea kuwa pamoja nasi na kutusaidia tunaposafiri, kila mmoja wetu. Tupe nguvu Zako za kufunga na ile—imani ya kujua ya kwamba Uwepo Wako usiashindwa utakuwa pamoja nasi. Katika saa hiyo ambapo hatuwezi kujisaidia, tunajua "Malaika wa Mungu wamepiga kambi juu ya wale wamchao, nnao watatuchukua ili wakati wo wote tusije tukajikwaa miguu yetu katika jiwe. Nasi tunaomba sasa ya kwamba utatupa baraka Zako kwa ajili ya Neno, na kunena kupitia kwetu, na ndani yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

4 Ninashukuru ya kwamba nuru ya jua la nje, jua la sayari, linaangaza. Ilikuwa mbaya sana asubuhi ya leo. Nami nafikiri katika nchi hii hasa, tuna utusitusi mwingi, hali ya hewa inayochosha. Na kuona jua likiangaza, likitoka, ni vizuri sana.

Maskini kule kuunganika kwa familia leo, nimekutana na ndugu zangu, nao wako nyumbani kwa dada yangu, na baadhi ya jamaa zetu karibu na mji na kila mahali. Kuna kundi kubwa la Wabranham. Kama wangalikutanika kutoka Kentucky, na hapa, nakisia ingetulazimu kukodisha mji mzima; ni wengi sana. Lakini kulikuwa kurudi nyumbani kudogo tu. Tulizoea kukutana kwa Mama naye alikuwa kama kizingiti kinachotuunganisha pamoja, cha fadhili. Bali Mungu alichukua hicho kizingiti kinachounganisha Mbinguni, nami natumaini ya kwamba sisi sote tutakutanika huko siku fulani.

5 Na sasa nilinena hivi majuzi, nikasema, "Unajua, ninaamini ya kwamba nita—nitapunguza jumbe zangu za Jumapili kufikia dakika ishirini, na—na, ama thelathini, kisha niwaombe wagonjwa." Nami niliwazia jambo hilo asubuhi ya leo.

Mami nikafikiri usiku wa jana wakati Dada Downing aliponipigia simu na kusema—akampigia simu Billy na kusema ya kwamba yeye na Dada Ungren wakiendesha barabarani waliteleza barabarani na motokaa ikaharibika. Na Billy alipokuwa angali dirishani, hapo, sijui ilikuwa saa ngapi; labda asubuhi ya leo, wakati fulani. Nilikuwa nimelala kwa muda mrefu kidogo. Nikaangalia kwa Ndugu Wood; taa zilikuwa zimezimwa. Nami nikapiga magoti tu kuomba, na nilipofanya hivyo, kitu Fulani kiliniambia tu, "Ni sawa." Kwa hivyo basi nikamwambia Billy, "Mwambie, 'kila kitu', nilifikiri, 'kingekuwa shwari.'" Nina furaha sana kuwaona asubuhi ya leo, na kuketi katika nyumba ya Bwana, huku nyuma baada ya kuwa barabarani.

Watu wanaokupenda kiasi hicho, kuja kwa mamia ya maili kuisikiliza Injili, ndipo nikawazia, "Ujumbe wa dakika ishirini, na kadiri ninavyonena polepole, usingefaa kitu." Kwa hiyo nilifikiri ningekuwa tu ... urefu huo.

Kwa hiyo basi, msikie Ndugu Ungren, mwanawe, asubuhi ya leo, akiimba, "Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu." Yeye ana ... Yeye ana maana zaidi kwake asubuhi ya leo kuliko ilivyokuwa jana alasiri, kwa sababu Mungu mkuu wa Mbinguni aliwaokoa mama na dada yake wa thamani, wapendwa.

6 Sasa, leo, tunatarajia wakati mkuu katika Bwana. Nami nilikuwa na vifungu viwili ama vitatu mbalimbali hapa ambavyo nilikuwa nikiangalia, wala sikuweza, nisingeweza kufikiria ni lipi ningezungumzia asubuhi ya leo. Moja lilikuwa Mtwikeni Yeye fadhaa zenu, kwa maana Yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu. Sasa, kama Yeye anajali, mbona wewe usijali?"

Kwa hiyo basi lingine, Billy Paul, ama si Billy Paul ... Mwanangu, Joseph, aliniletea fungu hili muda mrefu uliopita. Alikuwa ameketi chumbani siku moja, naye akasema, akiangalia kwenye picha, na Billy ... Ama, Joseph anapenda sana mitumbwi, kama wavulana wadogo; mitumbwi na farasi, mnajua. Naye akaniambia, "Baba, je! Yesu ana mtumbwi?"

Nami nikasema, "Sijui."

7 Kwa hiyo basi baada ya yeye kusimama na kutoka nje, ilitokea kuwazia, "Je! Yeye ana mtumbwi?" Nami nikachukua somo kutoka hapo, na kuliandika tu hapa kwenye kitabu changu, "Je! Yesu ana mtumbwi?" Na ikatokea kwamba niliwazia. Alipokuwa hapa duniani, ilimbidi kukopa tumbo la uzazi kuzaliwa, kaburi la kuzikwa, mtumbwi wa kuhubiri, bali Yeye ndiye Nahodha wa ile meli ya kale ya Sayuni. Hakika, Yeye anao. Lakini katika vile vifungu nilivyokuwa nikifikiria, nikawazia labda ningevipata baadaye, kabla hatujaondoka kurudi.

Mnajua, ninapenda kuzungumza kutoka kwenye maskani hapa, kwa sababu ni kanisa letu wenyewe. Tunajisikia huru kusema cho chote asemacho Roho Mtakatifu. Katika mahali pengine, hata ingawa mtu huyo ataka ujisikie huru, unajisikia umesongwa kidogo kwa sababu ukot—uko katika kanisa la mtu mwingine, nawe unataka kuwa muungwana kutosha kuheshimu yao—mawazo yao na mafundisho

8 Nilikuwa na wakati mzuri sana juma hili kule kwa Ndugu Burcham pale. Nami nikaingia kiwandani ambako walitengeneza jibini. Namwona yeye, mkewe, mwanawe, na wengineo wamo humu asubuhi ya leo. Kila mara nimefikiri kiwanda cha jibini kingekuwa kama mahali pengine nimetembelea, loo, panateleza na pachafu. Jamani, naweza kusema jambo moja, bila shaka mnaweza kuhakikisha mahali hapo si chafu. Hapo ndipo palipokuwa mahali paliposafishwa sana nilipopata kuingia, na hasa katika kiwanda fulani. Nami sikutambua; Nilifikiri, loo, labda watatengeneza ratili mia moja za jibini kwa siku. Nao wanatengeneza tani sita kila siku, na viwanda vitatu vinaendelea. Nikawaza, "Loo, jamani, ni nani anayekula jibini hizo zote?"

Lakini Bwana amembariki mtu huyu. Nilikuwa na majaliwa ya kuwa nyumbani kwake, nyumba ya kupendeza sana, mke mzuri aliyewekwa wakfu. Na hakuna sababu kwa nini hawapaswi kuishi kwa ajili ya Kristo kila siku, kama wanavyofanya. Nilikutana na wanawe, nao ni watoto wazuri sana. Tunashukuru sana kwa ajili ya ushirika huu ambao tunao mmoja kwa mwingine.

Niligundua kwamba mchungaji wao wa zamani alikuwa m—mtu ninayemjua, Ndugu Gurley, mtu mzuri sana wa imani ya United Pentekoste, ambaye nilikutana naye miaka mingi iliyopita, Jonesboro, Arkansas. Na sikujua ya kwamba walikuwa ... huyo alikuwa ni mchungaji wake, hata hivyo.

9 Sasa kumbukeni ibada za jioni hii. Halafu basi, Bwana akipenda, Jumapili ijayo tena tunatarajia kuzungumza. Na halafu nafikiri Jumapili itakayofuata basi sina budi kwenda Chicago. Ndipo nitakuwa nimeondoka kwa kitambo kidogo, sina budi kuirudisha familia nyumbani, kurudi, ama kurudi Arizona ili kwamba wao, watoto, waweze kujiandikisha shuleni tena. Na ndipo tukaacha kumsumbua mchungaji, kuchukua ibada zake.

Kwa hiyo, kwa hiyo tunamshukuru sana Ndugu Neville kwa ukarimu wake, mnajua, wa—wa kunialika. Naye yuko hivyo, siyo ... Ninapenda, ndugu, mtu kama huyo, ambapo hakuna hila, hakuna ubinafsi, ni Ukristo halisi tu. Ninapenda jambo hilo.

10 Sasa tutasoma baadhi ya Maandiko kisha kuyafafanua. Nami sijui ni wakati gani tutatoka, kwenye Jumbe hizi ndefu, bali nafikiri ... Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi kuhusu kuzungumza kwa muda mrefu sana, na mtu fulani akasema, "Vema, sasa, kama—kama ulinena tu kwa dakika chache; na unanena kwa namna fulani katika mafumbo, hata hivyo," kasema, "sisi—tusingeweza kamwe kuelewa." Kasema, "Endelea tu kuzungumza, na halafu punde si punde inafahamika." Yeye akasema. Kwa hiyo labda Bwana anatutaka tufanye hivyo.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu tena.

11 Bwana, Neno Lako liko wazi mimbarani na tukitambua ya kwamba pana siku litafungwa kwa mara yake ya mwisho, kisha hilo Neno litafanyika mwili. Na basi tuna—tunashukuru kwa ajili ya wakati huu asubuhi ya leo. Na utufungulie kwa Roho Mtakatifu Wako, yaliyomo katika Neno hili tutakalosoma. Jalia Roho Mtakatifu atufundishe leo mambo ambayo tunapaswa kujua. Na jalia sisi basi, kwa upande wetu, tusikilize kwa makini kila Neno, tulipime kwa kina. Na halafu basi wale wanaosikiliza kwa njia ya kanda, na wasikilize kwa makini. Na jalia tuweze kupata kile Roho Mtakatifu anachojaribu kutufunulia. Kwa kuwa tunatambua, kama Yeye anatupaka mafuta, basi upako huo siyo bure. Ni kwa kusudi fulani, kusudi lipate kutenda mema, kwa Bwana. Na jalia mioyo yetu na ufahamu uwe wazi, Bwana.

Na tuwe na uhuru wa kunena, na uhuru wa kusikia, na njia ya kuifikia imani kuamini yale ambayo tumesikia yakitoka katika Neno la Mungu, yapate kutupa Uzima wa Milele katika ile siku kuu ijayo. Tubariki leo. Tuhukumu tunapokosea. Hebu na tujue makosa tuliyo nayo. Na utubariki katika njia iliyo sahihi, tupate kujua njia ya kwenda, na jinsi ya kutenda katika ulimwengu huu wa sasa; ili kwamba tupate kuleta heshima, katika kuishi kwetu hapa, kwa Yesu Kristo, Ambaye alikufa apate kutupa Uhai katika maisha ya baadaye. Tunaomba hili katika Jina la Yesu. Amina.

12 Sasa ninataka kusoma kutoka sehemu mbili tu kutoka katika Maandiko, asubuhi ya leo. Na moja ya hizo inapatikana tu katika Kitabu cha Kutoka. Kwa kweli, zote mbili haziko kwenye Kitabu cha Kutoka. Moja, mlango wa 13, na kifungu cha 21 na cha 22. Na nyingine inayofuata ni sura ya 14, aya ya 10, 11

na 12. Sasa nitasoma kutoka Kutoka 13:21.

BWANA naye akawatangulia mchana ndani ya wingu mfano wa Nguzo, ili awaongoze njia; na usiku, ndani ya moto mfano wa nguzo, ili kuwapa nuru; wapate kusafiri mchana na usiku:

Ile nguzo ya wingu haikuondoka mchana, wala ile nguzo ya moto haikuondoka usiku, mbele ya hao watu.

Sasa katika Kutoka 14, na aya ya 10.

Hata Farao alipokaribia, wana wa Israeli wakainua macho yao, na tazama, Wamisri wanakuja nyuma yao; wakaogopa sana; wana wa Israeli wakamlilia BWANA.

Na ndipo akasema ... Musa, Kwa sababu kuna ... (samahani)

Wakamwambia Musa, Je! kwa sababu hapakuwa na makaburi katika Misri umetutoa huko ili tufe jangwani? Mbona umetutendea haya, kututoa katika nchi ya Misri?

Neno hili silo tulilokuambia huko Misri, tukisema, Tuache tuwatumikie Wamisri? Maana ni afadhali kuwatumikia Wamisri kuliko kufa jangwani.

Nitasoma vifungu vingine kadhaa.

Musa akawaambia watu, Msiogope ...

Sasa sikilizeni kwa makini hapa.

... Musa akawaambia watu, Msiogope, simameni tu, mkauone wokovu wa BWANA atakaowafanyia leo; kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele.

BWANA atawapigania, nanyi mtanyamaza ... BWANA akamwambia Musa, Mbona unanililia mimi? Waambie wana wa Israeli waendeleo mbele:

Nawe inua fimbo yako, ukanyoshe mkono wako juu ya bahari, na kuigawanya;, nao wana wa Israeli watapita kati ya bahari katika nchi kavu.

Nami, tazama, nitaifanya mioyo ya Wamisri kuwa migumu, nao wataingia na kuwafuatia, nami nitajipatia utukufu kwa Farao, na kwa jeshi lake lote, kwa magari yake na kwa wapanda farasi wake.

Na Wamisri watajua ya kuwa mimi Ndimi BWANA, nitakapokwisha kujipatia utukufu kwa Farao, na magari yake, na farasi zake.

Kisha malaika wa Mungu, aliyetangulia mbele ya jeshi la Israeli, akaondoka akaenda nyuma yao, na ile nguzo ya wingu ikaondoka hapo mbele yao, ikasimama nyuma yao.

Ikafika kati ya jeshi la Misri na jeshi la Israeli; ... napo palikuwa na lile wingu na lile giza, lakini lilitoa nuru wakati wa usiku; na hawa hawakuwakaribia hawa usiku kucha.

Musa akanyosha mkono wake juu ya bahari; BWANA akaifanya bahari irudi nyuma kwa upepo wa nguvu utokao mashariki, usiku kucha, akaifanya bahari kuwa nchi kavu, maji yakagawanyika.

Wana wa Israeli wakaenda ndani katika nchi kavu; nayo maji yalikuwa ukuta kwao mkono wa kuume, na mkono wa kushoto.

Na wale Wamisri wakafuatia, wakaingia ndani kati ya bahari, farasi zote za Parao, na magari yake, na wapanda farasi wake.

Ikawa katika zamu ya alfajiri, BWANA akalichungulia jeshi la Wamisri katika ile nguzo ya moto na ... ya wingu, akalifadhaisha jeshi la Wamisri.

Akayaondoa magurudumu ya magari yao, hata yakaenda kwa uzito; na Wamisri wakasema, Na tukimbie mbele ya Israeli; kwa kuwa BWANA anawapigania, kinyume cha Wamisri.

13 Neno la Bwana ni kuu sana, zuri sana, hakuna njia tu ya kuacha kulisoma. Linakuwa tu Uzima, tunapolisoma. Nafikiri, katika somo hili asubuhi ya leo, ingawa linanaswa, ninataka kusema jambo hili mwanzoni, inaonekana, ninajikuta mwenyewe. Na sababu yangu ... Jana nilipokuwa nikisoma—nami nikalipata hili somo, basi niliwaza, "Mimi, Bwana akipenda, nitanena kuhusu hilo kwa sababu linanisukuma chini." Nami natumaini linatusukuma sote chini tupate kuona, na itufanye kuinua macho yetu, na kusoma

kidogo kulinganisha siku hiyo ... na siku hii.

14 Ninataka kuchukua maneno matatu kwa ajili ya somo, na hayo ni: *Kwa Nini Unalilia? Nena!* Mungu alimwambia Musa, hapa katika kifungu cha 15, "Mbona unalilia Mimi? Nena na watu, wapate kusonga mbele." Na: *Kwa Nini Unalilia? Nena!*

Sasa, tuna somo kabisa, nami nitajaribu kuharakisha kupitia upesi iwezekanavyo, Roho Mtakatifu aongozavyo. Nami nataka kuwazia juu ya ... ya fungu hili la maneno, la Musa akimlilia Mungu, katika wakati wa shida; na Mungu akimkemea Musa arudi, papo hapo wakati shida ilipokuwa—inaanza. Na ni maumbile tu, inaonekana kana kwamba, kwa mtu kulia. Basi ni—ni karipio jinsi gani kwa Mungu kugeuka na kumkaripia kwa kusema hivyo, kwa kumlilia Yeye. Inaonekana kana kwamba ni jambo gumu sana.

15 Mara nyingi tunapoyaangalia Maandiko, kwa njia yetu wenyewe ya kuangalia, yaonekana ni magumu sana. Bali tukisoma kwa bidii punde tu, tutaona ya kwamba Mungu mwenye hekima yote anajua kile hasa anachofanya. Naye anajua jinsi ya kufanya mambo haya na jinsi ya kumshughulikia mwanadamu. Yeye anajua yaliyo ndani ya mwanadamu. Yeye, Yeye anamjua. Hatujui. Tunajua tu kwa akili zetu. Yeye anajua kilicho katika mwanadamu.

Musa alizaliwa katika ulimwengu huu, na mvulana mwenye kipawa. Yeye alizaliwa awe nabii, mkombozi. Alizaliwa na vifaa hivyo ndani yake alipozaliwa, kama vile kila mtu ajaye ulimwenguni huzaliwa na vifaa hivi, kama ninavyoamini kabisa katika—katika kujua kwa Mungu tangu asili, kule kuchaguliwa tangu asili.

16 "Si eti kwamba Mungu anapenda mtu ye yote apotee, bali wote wafikie toba." Lakini, akiwa Mungu, ilimbidi kujua, na anajua, "kujua mwisho tangu mwanzo." Mnaona? Asipofanya hivyo, basi Yeye hana kikomo; na kama Yeye si asiye na kikomo, Yeye si Mungu. Kwa hivyo hakupenda, bila shaka, mtu ye yote apotee, bali Yeye, akijua ni nani atakayepotea, na ni nani hangepotea. Hiyo ndiyo sababu, kusudi halisi la kuja kwa Yesu duniani, kulikuwa kuwaokoa wale Mungu, kwa kujua Kwake tangu asili, aliwaona na akataka waokolewe, mnaona, kwa sababu ulimwengu wote ulikuwa umehukumikiwa. Nami sioni jinsi tungalifundisha hayo kwa njia nyingine ye yote ila kujua kwa Mungu tangu awali, na Biblia inasema dhahiri kwamba Yeye "ajua mwisho tangu mwanzo" na anaweza kuunena.

Kwa hivyo, wakati m—mtu anapojaribu kujifanya kitu wasicho, wanafanya muigizo tu, na punde ama baadaye hakuna budi watatambulikana. Dhambi zako hukupata. Huwezi kuzifunika. Kuna kifuniko kimoja tu cha dhambi, hiyo ni Damu ya Yesu Kristo, na haiwezi kupakwa isipokuwa Mungu amekuita tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo ndiyo sababu hiyo Damu ilimwagwa; si kukanyagwa, na kufanyiwa mzaha, na—na kutaniwa, na—na kuzungumziwa vibaya, na—na kadhalika. Ilikuwa kwa kusudi halisi. Hiyo ni kweli. Si ya kuchezewa, si ya kuigizwa, kwa kusema ya kwamba dhambi zinafunikiwa wakati hazijafunikiwa. Na hamna mtu anayeweza kufunikiwa dhambi isipokuwa jina lake liliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yesu alisema, Mwenyewe, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote Baba alionipa, wakati uliopita, "alinionipa Mimi, watakuja Kwangu." Hiyo ni kweli. Kwa hivyo hauwezi ukafanya maneno hayo yaseme uwongo. Hayo yako pale kwa ajili ya Kweli na kwa ajili ya kusahihisha.

17 Naye Musa alizaliwa na karama ya imani; imani kuu aliyokuwa nayo Musa. Tunaiona, baada ya kitambo kidogo, likitokea ndani yake. Naye alizaliwa katika familia kuu, kama tunavyojua jinsi ambavyo baba yake na mama yake, na wanatoka katika familia ya Lawi. Ambapo, hadithi hapa, iliyotangulia jambo hili, katika Kitabu cha—cha Kutoka, ikisimulia vizuri sana maisha ya mtu huyu mashuhuri. Naye alikuwa mmoja wa wa—wahusika wakuu sana wa Biblia, kwa kuwa alikuwa ni mfano halisi wa Bwana Yesu.

Yeye alizaliwa katika uzazi wa kipekee sana, kama Bwana Yesu. Alizaliwa katika wakati wa mateso, kama Bwana Yesu. Alizaliwa apate kuwa mkombozi, kama Bwana Yesu. Alifichwa na wazazi wake, mbali na adui, kama Bwana Yesu. Naye akaja kwenye wakati wake wa huduma, kama Bwana Yesu. Alikuwa kiongozi, kama Bwana Yesu. Yeye alikuwa ni nabii, kama Bwana Yesu. Naye alikuwa mtoa sheria, kama Bwana Yesu.

Nasi tunaona ya kwamba alikufa kwenye Mwamba, na hapana budi alifufuka tena na kila kitu, kwa sababu, miaka mia nane baadaye alikuwa amesimama juu ya Mlima wa Kugeuzwa, akizungumza na Bwana Yesu. Mnaona? Malaika walimchukua. Hakuna mtu ajuaye mahali alipozikwa. Hata ibilisi hakujua jambo hilo. Kwa kweli, siamini aliwahi kuzikwa. Na—naamini ya kwamba Mungu alimchukua, naye—naye akafa kwenye ule Mwamba ambao alikuwa ameufuata siku zote za maisha yake.

Naye alikuwa ni mfano mkamilifu wa Kristo. Alikuwa ni mfalme juu ya watu. Yeye alikuwa mtoa sheria. Yeye alikuwa a—alikuwa m—mtu wa kuwahifadhi wa watu. Yeye alikuwa kila kitu, katika—katika mfano, wa alichokuwa Kristo.

18 Sasa basi tazama ya kwamba alizaliwa akiwa na karama yake kuu na sifa ndani yake, bali ilichukua tu kitu fulani kukumulika, kukifanya kitu hicho Hai.

Mnaona, mbegu ya Mungu hakika iliwekwa ndani yetu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na wakati hiyo Nuru inapogusa hiyo mbegu, inaifanya Hai, bali Nuru haina budi kwanza kuiangazia ile mbegu.

Kama vile nimefundisha mara nyingi juu ya maskini mwanamke yule kisimani, yeye akiwa katika hali hiyo. Ingawa yeye alikuwa m—mtu mwenye sifa baya, ingawa maisha yake—yake yalikuwa yameshushwa, naye alikuwa katika hali hiyo kwa sababu mapokeo hayakuwa yamemguza kamwe, lakini, ingawa, wakati hiyo Nuru ilipomgusa kwanza, mara akaitambua, kwa sababu kulikuwemo kitu fulani mle kuiitikia. "Wakati kilindi kinapoita Kilindi," hapana budi kuwe na Kilindi mahali fulani cha kuitikia wito huo.

Naye Musa hapa alizaliwa huyu nabii, bali alilewa katika shule ya wenye akili na nyumbani mwa Farao. Farao Seti, aliyelewa chini yake, alikuwa mtu ambaye bado alikuwa mwenye kuheshimu, na aliamini Yusufu kuwa nabii wa Mungu. Lakini akaja Ramesesi baada ya Seti, na Ramesesi hakujali kuhusu Yusufu. Na kwa hiyo, kwa hiyo, hapo ndipo shida ilipoanza, sasa, wakati Farao alipoinuka ambaye hakumjua Yusufu.

Lakini sifa hizi kuu, hebu tuzizungumzie kwa muda kidogo tu, na, kabla hatujafikia sehemu kuu ya somo. Nina njia ya kipekee ya kuanzisha somo na kulifafanua, na Bwana atusaidia asubuhi ya leo tunapolifafanua.

19 Musa, akizaliwa na karama hii kuu ya imani. Ndipo, alitiwa mafuta na kuagizwa kwenye kijiti kilichowaka moto, kuwakomboa watu wa Mungu. Sasa, tunaona jinsi mtu huyu alivyokuwa na sifa kuu! Yeye alizaliwa kwa ajili ya jambo fulani. Mungu alikuwa na kusudi ndani yake.

Mungu ana kusudi la wewe kuwa hapa. Mnaona? Iwapo unaweza tu kuwa, kufikia mahali hapo, ni shida nyingi vipi utamwondolea Mungu pamoja nawe, pia.

Musa akazaliwa, kisha alikuwa, baadaye akaletwa mahali alipotiliwa mafuta. Na tazama mbegu ile imekaa pale kwa mawazo ya kiakili, pamoja na imani yote aliyozaliwa nayo kuwakomboa watu hawa, hata hivyo haikuwa Hai hata hiyo Nuru kutoka kwa Kijiti Kilichowaka Moto ilipoimulika; hata alipoona, si kitu ambacho alikuwa ameshasoma habari zake, bali kitu alichokuwa ameona kwa macho yake; Kitu kilichomzungumzia, naye akakizungumzia. Loo, jinsi hilo lilifanya mambo yawe Hai.

20 Nafikiri mtu yeyote aliye na ... ama mwanamke, mvulana ama msichana. Na ninafikiri katika mawazo ya kiakili ya yale wanayodhani Neno lilivyo, na kadhalika, hawawezi kamwe kuwa na msingi imara hata watakapokutana na hiyo Nuru ambayo hulifanya Neno kuwa kweli.

Nafikiri hamna kanisa katika taratibu zake, haidhuru ni la kiakili na msingi vipi, kanisa hilo haliwezi kusitawi hata ya kimbinguni yamejulikana miongoni mwa watu wale, nao wayaone. Kitu fulani wanachoweza kuzungumzia, ambacho kitawajibu, ambacho huthibitisha Neno hili lililoandikwa.

21 Sasa kumbuka, wakati Musa alipokutana na kijiti hiki kilichowaka moto, hilo Neno lilithibitishwa kabisa. Ilikuwa ni Neno. Musa hakupaswa kuwa na wasiwasi, "Sauti hii inamaanisha nini? Kiumbe hiki ni kitu gani hapa?" Maana tayari Mungu aliisha andika kwenye Maandiko, katika Mwanzo, ya kwamba, "Watu wako watakuwa wageni katika nchi hii ya kigeni, bali watarudishwa baada ya miaka mia nne, watarudi nchini humu tena, kwa maana hauja—haujatimbia uovu wa Waamori bado." Sasa, mamia na mamia ya miaka hapo kabla, Mungu alikuwa amesema ya kwamba, "Israeli wangekaa na kutendwa vibaya katika nchi ya kigeni, na wangekaa huko miaka mia nne. Lakini Mungu, kwa mkono wenye nguvu, angewatoa." Kwa hiyo, mnaona, pamoja na kijiti hiki kinachowaka moto ...

Musa alijua jambo hili, kiakili. Na mbegu iliyozaliwa ndani yake, ilikuwa moyoni mwake. Naye alijaribu, kupitia ujuzi wake wa kiakili pamoja na Neno, kujaribu ku—ku—kuwatoa, kuwakomboa, kwa sababu alijua alizaliwa kwa kusudi hilo. Alijua huo ulikuwa, wakati Maandiko yote yalisema wao tayari walikuwa wamekuwa huko kwa miaka mia nne.

Kama tu tujuavyo sasa, kama vile mtu mmoja alivyoniuliza muda mchache uliopita, kuhusu kule Kuja na Kunyakuliwa. Tunajua. Tunajua ya kwamba wakati umekwisha, wakati wa Kunyakuliwa umewadia, nasi tunatazamia imani ya kunyakuliwa inayoweza kuunganisha kanisa na kulipa nguvu fulani za kimbinguni, zinazoweza kuigeuza miili hii tunamoishi. Tunamwona Mungu anayeweza kumfufua aliyekufa akainuka kutoka sakafuni ama nje uwanjani, na kumfanya hai tena na kumleta mbele zetu, tunapomwona Mungu anayeweza kuchukua kansa ambayo imemla mtu akawa kivuli na kumwinua akawa mtu mwenye nguvu na afya, hiyo inapaswa kuwapa watu imani ya kunyakuliwa. Kwamba, wakati hiyo Nuru itakapomulika kutoka angani, na parapanda ilie, ule Mwili wa Kristo utakusanywa pamoja, na kufumba na kufumbua kubadilishwa, na kuchukuliwa Mbinguni. Naam, lazima kitu kama hicho kitendeke. Na shule zetu za theologia haziwezi kamwe kutoa hayo, ingawa wao kiakili wako sawa. Bali huna budi kukutana na Nuru hiyo! Huna budi kupata hicho kitu.

22 Na hapa Musa, akiweka msingi wa wito wake mkuu juu ya Neno, na ulikuwa mkuu, hata siku moja akakutana na Nuru hii, na Neno lenyewe likazungumza naye. Ndipo akapata upako wake. Hiyo ilipaka mafuta kile alichokuwa nacho ndani yake, kile kilichokuwa ndani yake, zile—zile akili zilizoamini, ile imani

iliyoweka msingi juu ya imani yake katika Mungu, ambaye alimtenga na mama yake. Na sasa alipofika kwenye hiyo Nuru, ikatia upako hiyo hata akaamini. Mnaona? Ni upako ulioje! Naye akaagizwa.

Sasa, tunajua, kiakili alikuwa amemsikia mama yake. Alijua kitakachotukia, naye alijua alikuwa akiishi katika siku hiyo. Bali hapa akatambua kwamba yeye alikuwa ameshindwa, kwa hivyo huenda aka...imani yake huenda ilikuwa imefifia kidogo. Lakini basi wakati anapokuja kwenye kile kijiti, Mungu alisema, "Nimesikia kilio cha watu Wangu, nami ninakumbuka ahadi Yangu kwa baba zao, Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, nami nimeshuka." "Mimi," pale, ki—kiwakilishi nafsi, "Nimeshuka kuja kuwakomboa."

23 Na sasa, na hebu niongezee tu hili kama ... Mungu anisamehe kama inasikika kama kukufuru. "Mimi sitendi kazi duniani, kupitia tu kwa mwanadamu. Mimi—mimi—mimi ni Mzabibu; nanyi ni matawi. Na Mimi hujijulisha Mweyewe tu ninapoweza kumpata mtu, Nami nimekuchagua, nami ninakutuma uende ukawatoe." Mnaona? Sasa angalia, "Nitakuwa pamoja na kinywa chako, nami ... chukua fimbo hii."

Naye Musa akasema, "Je! Ninaweza kuona thibitisho ya kwamba utanituma, na Wewe umenitia mafuta, na Wewe utafanya mambo haya?"

Kasema, "Una nini mkononi mwako?"

Akasema, "Fimbo."

Kasema, "Itupe chini." Ikageuka ikawa nyoka. Akakimbia.

Akasema, "Ichukue." Iligeuka ikawa fimbo. Kasema, "Weka mkono wako kifuni mwako." Akautoa, nao ulikuwa ukoma. Rudisha, na uliponywa.

24 Kasema, "Yeye aliuona utukufu wa Mungu." Hakukuwa na swali lingine tena, kwa Musa. Je! Ulipata kuona, yeye hakukimbilia nyikani tena? Alijua alikuwa ametiwa mafuta. Alijua ambapo, mambo haya yote yaliyokuwa moyoni mwake, Hizi sifa kuu nzuri, naye ... zilikuwa zimetiwa mafuta sasa. Yeye, yeye yuko tayari. Yuko tayari kwenda. Kwa hiyo anashuka kwenda Misri.

Mungu alikuwa amesema, "Nitakuwa pamoja nanyi," kwa hiyo hilo—hilo latosha. Kama, "Nitakuwa pamoja nawe," hayo tu ndiyo Musa aliyopaswa kujua, kwa ajili ya wito huu mkuu moyoni mwake. Na sasa Mungu alisema, "Nitakuwa pamoja nanyi."

Sasa, Mungu pia alikuwa amethibitisha madai yake, ya Musa. Madai ya Musa, "Nilikutana na Bwana. Naye akasema niwaambieni, 'MIMI NIKO' alinituma." Mnaona?

Basi wakasema, "Hapa kuna mtu, Myahudi mwingine, labda baadhi ya hawa washupavu wa dini ambao wamekuwa wakija wakati wote wakiwa na mpango fulani wa kututoa utumwani." Nanyi mwajua jinsi watu walivyo wanapokuwa watumwa ama utumwani kwa ajili ya jambo fulani, kila mara kuna mjaja fulani anaowajia, mnajua, kutenda hayo.

Kwa hiyo, Musa, Mungu alimwahidi Musa, "Nitakuwa pamoja nawe. Nitakuwa ndani yako. Maneno Yangu yatakuwa Maneno yako. Wewe nena Maneno Yangu na useme tu yale Nisemayo."

25 Na sasa Musa aliposhuka akaenda na kuwatolea mwito huu na kusimama mbele ya Farao na kumwambia Bwana Mungu wa Waebrania amesema, "Watoe hao watoto." Naye hangewaruhusu waende. Kwa hivyo a—kafanya ishara mbele ya wazee na mbele ya Farao, na ishara alizozitenda Mungu. Yeye alisema, "Sasa, kesho, yapata wakati huu, jua litatua. Kutakuwa na giza kote Misri," na ikatimia kabisa. Na ndipo akasema, "Kuna—wanakuja nzi juu ya—juu ya nchi," naye akanyosha fimbo yake na kuwaita nzi, na nzi wakaja. Naye alitabiri, na kila kitu alichotabiri kilitendeka jinsi hasa. Ilikuwa ni Mungu. Mnaona?

26 Mungu alikuwa amemwita tangu kuzaliwa kwake, akaweka sifa ndani yake, ya imani kuu, kisha akashuka na Uwepo Wake na kutia mafuta kitu hicho kikuu ndani yake, na kumtuma chini na Neno Lake, naye alikuwa amethibitishwa ipasavyo madai yake. Haidhuru ni walaghai wangapi waliinuka, ni mangapi ya mambo haya mengine yalikuwa yametendeka, Mungu alikuwa akinena kwenye ... Musa alitambulishwa. Musa, yale Musa aliyosema, Mungu aliyaheshimu. Nawatakeni msisahau Neno hilo kamwe. Yale Musa aliyosema, Mungu aliyaheshimu, kwa sababu Neno la Mungu lilikuwa ndani ya Musa. "Nitakuwa pamoja na kinywa chako; Utanena mambo ya kweli." Sasa, yale Mungu asemayo—yale Mungu asemayo, Yeye huyanena kupitia Musa, na hiyo iliimarisha na kuthibitisha madai yake.

27 Pia, aliambiwa na mama yake kuhusu uzazi wake usioelezeka, na jinsi wakati ulikuwa umewadia karibu na ile saa ambapo kungekuwa na mkombozi. Amramu na—na Yokebedi, mwana na binti wa Lawi, wakaanza kumwomba Mungu kumtuma mkombozi. Na inachukua...unapona wakati wa ahadi umekaribia, inawafanya watu waanze kuomba na kuona njaa. Na hapana shaka ya kwamba—ya kwamba Yokebedi alikuwa amemwambia mara nyingi, mama yake; kama alivyokuwa mwalimu wake, pia, kama tunavyojua hadithi hiyo. Na alikuwa amemwambia jinsi alivyokuwa ameomba. "Na, Musa, ulipozaliwa, mwanangu, ulikuwa mtoto maalum. Ulikuwa tofauti. Kuna kitu kilichotendeka katika kuzaliwa kwako."

Niliwafanyia watoto mchezo wa kuigiza, si muda mrefu uliopita, na kusema, "Wakati Amram alipokuwa chumbani akiomba, alimwona Malaika akichomoa upanga wake na kuuelekeza kaskazini, na kusema, "Utapata mwana, naye atawapeleka wale wana upande wa kaskazini hata kwenye Nchi ya Ahadi." Nikiwaonesha watoto wadogo mchezo wa kuigizwa kusudi wapate kuelewa, akili zao hazijafikia mahali mlipo ninyi watu wazima, ambapo unaweza kufahamu mambo ambayo Roho Mtakatifu huwafunulia.

28 Sasa, ingawa mama yake alikuwa amemwambia mambo haya, naye alijua jambo hili, hata hivyo alihitaji mguso mwingine. Ma—fundisho yalikuwa mazuri, bali alihitaji mawasiliano ya kibinafsi.

Hicho ndicho ulimwengu unachohitaji leo. Hayo ndiyo kanisa linayohitaji leo. Hicho ndicho kila mtu anachohitaji, hao ni wana na binti za Mungu. Ili kuwa hivyo, unahitaji mawasiliano ya kibinafsi, mnaona, Kitu fulani. Haidhuru, unajua Neno ni kweli, unajua ni kweli; lakini basi linapowasiliana, na halafu mnaona jambo hilo likitendeka, basi unajua uko kwenye njia sahihi. Mnaona? Na, angalia, daima itakuwa ni ya Kimaandiko. Itadumu na Maandiko kwa sababu hii ilifanya hivyo.

Maombi ya Amramu yalikuwa sawa kabisa na Maandiko. Maombi yao yalikuwa pamoja na Neno lililoahidiwa. Mungu aliahidi wakati huo kufanya jambo hilo. Waliomba kwa ajili ya jambo hilo, kisha hapa akazaliwa mtoto maalum. Nao ...

29 Angalia! Loo, jinsi ninavyopenda jambo hili! Mnaona, katika ile saa ambayo Farao alikuwa akiwaua watoto wote, mnaona, akiwaua kwa—kwa upanga, upanga wa mlinzi; wao, wao waliwachoma hawa watoto wadogo hadi wakafa, wakawalisha kwa mamba, miili midogo, hata mamba labda wakanona kwa miili ya watoto wa Kiebrania. Lakini Biblia ilisema, ya kwamba, "Wazazi hawakuogopa amri ya Farao ya kuwaua watoto." Hawakuogopa. Hawakuogopa, kwa sababu waliona kitu fulani katika mtoto huyu, kwa kuanzia. Walikiona, ya kwamba hili lilikuwa jibu la maombi.

Na sasa Musa alikuwa na haya yote kama msingi, kwa hiyo Musa alijua alitumwa kwa kusudi hasa la kuwakomboa wana wa Israeli.

Mnaona, malezi yote yanalundikana. Unapopata cho chote, na unaweza kuileta Biblia, ikisema, "Hii itatendeka," na hili hapa linatendeka; "Na hii itatendeka wakati huo," hapa inatendeka; "Na hii itatendeka katika wakati huo," hapo inatendeka; ndipo yote yanakusanyika pamoja na kutuchora picha.

30 Loo, jinsi haya Maskani asubuhi hii, jinsi sisi watu wa wakati huu, Ndugu Neville, tunapona mvi zikiingilia nywele zetu na mabega yetu yakiinama, tunapona ulimwengu ukijisokota-sokota na kuyumbayumba kama ulivyo, na jinsi tunavyoweza kutazama huku na kuona ile ahadi ikikaribia! Ni, ni ... Nafikiri, wakati mwingi, kama mtu ye yote angalirukia mara moja, bila kulielewa, ama angalielewa, hasa, aje kwake mara moja, nusura ingekupeleka katika Umilele, pamoja na tu...na jambo la kunyakulia! Wala kamwe sikujua jambo hilo, na tu, loo, kupitia mambo ambayo tumeona na kujua na kuelewa, na yote yanaruka kwa wakati mmoja. Mwanamume, ama mwanamke, mvulana, ama msichana, labda wangeinua mikono yao na kusema, "Hebu twende, Bwana Yesu," mnaona. Loo, jinsi hiyo saa ilivyo karibu!

31 Musa akijua ya kwamba alizaliwa kwa kusudi hilo, na akatazama nje ya madirisha na kuwaangalia hao Waebrania walipokuwa wakifanya kazi; akaangalia nyuma hapa katika Maandiko, nayo yakasema, "Nao watakaa ugenini miaka mia nne, mnaona, lakini nitawatoa kwa mkono wenye nguvu." Ndipo anaporudi, baada ya agizo, aliyetiwa mafuta, alijua ya kwamba alizaliwa ... Na imani yake angalia, kwa imani aliwaona hao watu na akajua walikuwa watoto wa Mungu, maana ulimwengu ... Ne—Neno lilisema hivyo. Hawakuwa wa ulimwengu, wala hawakuwa kama hao wengine. Walikuwa tofauti. Nao walikuwa wakorofi na washupavu wa dini, kwa ninii—uzuri wa kudanganya wa Misri; naye angekuwa mwana wa Farao, ambaye angetwaa huo ufalme, baadaye. Lakini, yeye, kulikuwako na kitu fulani ndani yake, i—imani halisi ambayo hakikuangalia mambo hayo, uzuri ambao angepaswa kuurithi. Yeye alitazama ahadi ya Mungu, naye alijua ya kwamba wakati ulikuwa unakaribia. Na yale mtu huyo lazima alifikiri!

32 Ninataka kuzungumza naye, siku moja, nitakapokutana naye upande ule mwingine. Unasema, "Huo ni wazimu, ndugu..." La, sivyo. Nitakutana naye, kwa neema ya Mungu. Naam, bwana. Nitazungumza naye, siku moja, Musa mwenyewe. Na jinsi ningetaka kumuuliza, vile tu, wakati alipoona kutayarishwa kwake!

Jinsi shetani angemhangaisha, akisema, "Ahaa, hao watu hawatakuamini. A-ha. Hamna—hamna kitu kama hicho,"

33 Lakini wakati mbegu hiyo ilipopata Uhai kule juu, kitu fulani kilimgusa, naye alijua kulikuwa na jambo fulani litakalotukia. Alijua. Akaangalia saa yake na kuona ilikuwa ni saa ngapi, naye alijua, na jinsi alivyopaswa kuwazia alipokuwa akiangalia. Sasa wakati alipokusanya haya yote pamoja, jambo hili lote kuu aliloona; wakati wa Maandiko, maombi ya mama yake na baba yake, naye alizaliwa kipekee, mtoto wa kipekee. Na, wakati wote, kulikuwako na kitu fulani huko chini ndani yake.

Na sasa anaondoka na kujaribu kufikiri angechukua mafunzo yake ya kijeshi kutoka shuleni kwake, na kuwakomboa watoto, na hilo lilishindwa.

Kisha anaenda zake jangwani na kumwoa m—msichana mrembo wa Kushi, nao wakampata mvulana mdogo aliyetwa Gershomu.

Na siku moja alipokuwa akichunga kondoo, mara akaona kichaka kikiwaka mlimani, kikiwaka moto. Naye akapanda kwenda kule. Wala Siyo mwenye akili, siyo ku—kuwazia, siyo madanganyo, siyo madanganyo ya macho, bali ndani yake ... Mlikuwemo Mungu wa Ibrahimu, katika Nuru, Nguzo ya Moto kule nyuma katika kichaka, huo moto, kama mawimbi ya nuru yaliyokuwa yakitoka, bali haukukisumbua hicho kichaka. Na Sauti ya Maandiko, Sauti ya Mungu, ilinena kupitia pale, na kusema, "Nimekuchagua. Wewe ndiwe mtu huyo. Nilikuinua kwa kusudi hili. Ninawathibitishia hapa, kwa ishara, utashuka kwenda kuwakomboa hao wana kwa sababu Neno Langu halina budi kutimizwa."

Loo, Neno Lake la siku hizi halina budi kutimizwa. Tunaishi katika wakati huo. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini; Neno halina budi kutimizwa. Mbingu na nchi zitapita, bali si Neno Lake.

34 Sasa, wakati Musa alipokusanya haya yote pamoja, na kuona kwa kila mwelekeo, ilitia mafuta imani yake. Amina! Loo, jamani! Ni wazo la jinsi gani! Hii, yenyewe, akaona kwa Maandiko ikionyesha kile ilichokuwa, na kule kunena kwa Mungu, na thibitisho lake pale, kuliitia upako imani aliyokuwa nayo, kwenda kutenda kazi.

Inapaswa kutufanyia nini? Tunahitaji toba. Tunahitaji ufufuo. Ninasema mwenyewe. Mnaona? Ninahitaji kutikiswa. Ninahitaji kitu fulani. Nilisema nilikuwa nikijizungumzia, ama kunena habari zangu mimi. Ni—ni—ninahitaji ku—kuamshwa.

Na ninapowazia juu ya lile thibitisho kuu, kila kitu kiliwekwa pale vizuri sana, na ikaitia upako imani ya Musa. Na, jamani, aliona hakuna kitu ...

35 Hapa, alikimbia kutoka Misri, na, kwa kweli, angeweza kuanzisha u—uasi ama kitu fulani, na angeweza—angeinuka na kuanzisha mapinduzi huko Misri, na angalichukua jeshi na kupigana, lakini, mnaona, na alikuwa na maelfu mengi upande wake. Lakini badala ya jambo hilo, yeye aliogopa hata kufanya jambo hilo, akiwa na majeshi upande wake.

Lakini sasa huyu hapa anarudi, miaka arobaini baadaye, umri wa miaka themanini, akiwa na fimbo tu mkononi mwake. Kwa nini? Kile kilichokuwa kikiwaka moyoni mwake kilikuwa kimekuwa halisi. Yeye alikuwa ametiwa mafuta wakati huo, naye alijua alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hakuna kitu kitakachomzuia sasa. Hakuhitaji jeshi lolote. Mungu alikuwa pamoja naye. Hayo tu ndiyo aliyohitaji; Mungu pamoja naye.

Loo, unapojua ya kwamba Mungu amekutuma kufanya jambo fulani, nawe unaliona likisongea pale, hamna kitu kinachoweza kupachukua mahali pake. Hivyo tu.

36 Nakumbuka nyakati ambazo Mungu ameniambia kuhusu mambo fulani ambayo yangetendeka, kisha nasonga mbele na kuyaona pale pale, jinsi ... Loo, ni hisia iliyoje! Hali hiyo tayari imedhibitiwa, hivyo tu, mnaona, kwa sababu Mungu alisema hivyo.

Nakumbuka, wengi wenu mnakumbuka kuhusu yule mvulana mdogo aliyefufuliwa kule Finland, halafu kutoka kwa wafu, alikuwa ameuawa na motokaa. Nami nilisimama pale kando ya barabara, na kuanza kuondoka kutoka kwa mtoto huyo, kisha nikageuka na kuangalia nyuma. Na kitu fulani kiliweka mkono wake begani mwangu, nami nilidhani ilikuwa ni Ndugu Moore, na hakuna mtu aliyekuwa karibu nami. Nami nikaangalia nyuma, kisha nikaangalia juu ya mlima niliouona. Nikasema, "Vema, nimeona mlima ule mahali fulani, bali hatukupitia humu. Tulipitia njia nyingine. Kilima hicho kiko wapi?"

Nami nikaangalia na kuona hilo gari kule chini, likiwa limeharibika; nikamwona huyo mvulana mdogo pale akiwa na ninii yake ... amelala pale akiwa na—kama kunyolewa nywele, kama tunavyokuita hapa. Macho yaligeuka nyuma, kama ya Ndugu Way yalivyokuwa siku moja alipoanguka. Na maskini mguu wake mdogo umejipenyeza kwenye soksi, ambapo miguu yake midogo ilivunjika. Na damu kutoka kwenye macho yake, na pua, na masikio. Kisha nikaona suruali yake ndogo, fupi; imefungwa kwa vifungo, hapa, kwenye kiuno chake kidogo; na soksi zake ndefu zimevutwa juu hivi kama tulivyokuwa tukizivalia miaka mingi iliyopita.

37 Nami nikaangalia kila mahali, na kulikuwa kabisa, jinsi hasa Roho Mtakatifu alivyokuwa ameniambia miaka miwili iliyopita, wakati ninyi nyote mliandika katika Biblia zenu kote nchini, kwamba jambo hilo lingetukia. Loo, hapo, basi, mambo yako tayari. Haidhuru yeye ni mfu jinsi gani; haidhuru mtu ye yote anasemaje; imekwisha. Hana budi kufufuka.

Nikasema, "Iwapo huyu mtoto hatafufuka kutoka kwa wafu, basi mimi ni nabii wa uongo, mimi ninamwakilisha Mungu kimakosa. Kwa kuwa, katika nchi ya uenyaji wangu, miaka miwili iliyopita, Yeye aliniambia jambo hili lingetukia. Na hapo hawa wahudumu na kadhalika, imeandikwa katika ukurasa wa kwanza wa Biblia zetu, na hii hapa hasa. Someni toka kwa ukurasa wa kwanza jinsi itakavyotukia katika nchi iliyojaa miamba, na kadhalika, na kadhalika, atauwa ... atakuwa upande wa kulia wa barabara." Nikasema, "Hiyo hapo. Hamna kinachoweza kuizuia." Hali tayari imedhibitiwa."

Imani iliyokuwa ndani ya moyo wangu ilikuwa imetiwa mafuta. Loo, laiti ningaliweza kueleza jambo hilo! Imani ambayo Mungu ... nilikuwa nayo katika Mungu, iliyoniambia, na haikushindwa kamwe, iliniambia, "Hali imedhibitiwa sasa. Hapa liko lile hasa nililowaonesha miaka miwili iliyopita, na ndilo hili hapa katika utaratibu kabisa. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kusema neno." Na huyo mvulana mdogo akafufuka kautoka kwa wafu. Mnaona?

38 Nilikuwa nikiwazia, na nikimwalia Ndugu Fred Sothmann anayeketi pale, na Ndugu Banks Wood na hao wengine. Hivi majuzi, kule kwenye Barabara Kuu ya Alaska, jinsi nilivyosimama kanisani na kuwaambieni ninyi nyote juu ya mnyama aliyeonekana kama kulungu mwenye pembe zenye urefu wafuti arobaini na mbili na dubu mwenye rangi ya fedha na kijivu. Sikuwa nimewahi kufika hapo hapo kabla, na jinsi ambavyo ninii ... ya kwamba ningepata hili, na jinsi ingekuwa, na ni wangapi wangukuwa pamoja nami, na jinsi wangevaa. Mnajua jambo hilo, kila mmoja wenu, majuma na majuma kadhaa kabla halijatukia.

Na pale nilipoenda kule, bila kujua, yule mnyama alikuwa amelala pale. Nami nikaenda, na—naye ... haingaliwezekana. Kama mwindaji angejua ama awe anasikiza kanda hii, jinsi ambavyo huwezi kwenda karibu na mnyama; angeruka na kukimbia. Lakini yeye hakufanya hivyo.

39 Ananing'inia pale katika chumba changu cha kusomea. Pale ananing'inia yule dubu mwenye rangi ya fedha, vile hasa tu. Na na—rula imo mle, utepe wa kupimia, kuonesha hasa... Na pembe itapungua angaa inchi mbili ama zaidi, wakati ingali bichi juu ya mnyama na wakati inapokauka, bali hii haikupungua kamwe. Ingali hizo inchi arobaini na mbili kabisa. Mnaona? Pale yualala yule dubu mwenye rangi ya fedha, ana urefu wa futi saba hasa na kila kitu vile hasa ilivyokuwa, yuko pale sasa.

Bali huyu mtu aliponiambia, "Sasa, tazama Ndugu Branham, tumempata huyu mnyama uliyenena habari zake, lakini ulituambia ungempata dubu mwenye rangi ya fedha na kijivu kabla hatujafika chini ya kilima, kurudi kule wale vijana wanaume, yule mwenye shati la kijani kibichi."

Nikasema, "Ni BWANA ASEMA HIVI. Mungu alisema hivyo."

"Lakini, Ndugu Branham," akasema, "Ninaweza kuona kila kitu hapa, kwa maili nyingi, hakuna kitu. Yeye anatoka wapi?"

40 Nikasema, "Hilo si langu kuhoji. Mungu alisema hivyo! Naye ni Yehova-Yire. Anaweza kumleta dubu kule. Angeweza kuweka mmoja pale." Naye alifanya hivyo. Na huyo hapo. Ni hali iliyodhibitiwa.

Basi Musa alipoona ya kwamba aliinuliwa kwa kusudi hili naye alikuwa amekutana na huyo Mungu aliye mkuu uso kwa uso aliyekuwa ametoa ule mwito, naye akamtia mafuta, na kumtambulisha, na kusema, "Huu ndio mwito, wako, Musa. Ninakutuma, nami nitakuonesha utukufu Wangu. Nami niko hapa, kwenye kichaka, nikiwaka moto. Shuka uende kule! Nitakuwa pamoja nanyi." Hata hakuhitaji fimbo. Alikuwa na Neno, Neno lililothibitishwa, na hapo akaenda. Ilitia upako imani iliyokuwa ndani yake.

Nayo inatutia upako tunapona ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, kuona ya kwamba hizi ishara zote tunazoonza zikitendeka, zimeandikwa katika Maandiko ya kwamba zitatendeka katika siku za mwisho; kote toka Mbinguni, hata kwenye nguvu za kisiasa, na tabia za watu, na upotovu wa ulimwengu, na kati ya wanawake, na jinsi wangepanya katika siku za mwisho, na jinsi wanaume wangetenda, na jinsi makanisa yangetenda, na jinsi mataifa yangetenda, na jinsi Mungu angetenda. Nasi tunaona yote yamewekwa papa hapa juu yetu.

Loo, inatia upako imani yetu. Inatutoa katika duara kubwa. Mnaona? Ina—inatutenganisha na mambo mengine ya ulimwengu. Mnaona? Haidhuru sisi ni wadogo iliyoje, ama jinsi tulivyo wachache, jinsi tunavyochekwa, kudhihakiwa, haileti tofauti hata kidogo. Hivyo tu. Tunaiona. Kuna kitu fulani ndani yetu. Tulichaguliwa tangu asili kuiona saa hii, na hamna kitu kitakachotuzuia kuiona. Amina! Hapa, Mungu amekwisha kunena. Ta—tayari imetendeka. Tunaiona. Loo, jinsi tunavyomshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hili! Loo, basi, inaonesha imani yako tunapona mambo haya yakitendeka hapa.

41 Sasa, hapa tena tunasoma ya kwamba, "Musa alihesabu ya kwamba kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri." Naam, yeye alihesabu ku—kushutumiwa Kwake Kristo.

Sasa kumbukeni, "kushutumiwa Kwake Kristo." Mnaona, kuna kushutumiwa katika kumtumikia Kristo. Kama unapendwa sana na ulimwengu, basi hauwezi kutumika, haumtumikii Kristo. La, huwezi. Kwa sababu, mnaona, kuna shutuma inayoambatana nayo. Ulimwengu ulishutumu daima.

Kule nyuma kabisa, maelfu ya miaka iliyopita, kulikuwa na shutuma iliyoambatana nayo. Naye Musa kuwa farao, alikuwa farao anayekuja, mwana wa Farao. Naye ndiye alikuwa Farao aliyefuata, mwenye kibali mbele ya watu, "na hata hivyo aliona ..." Kuhesabu maana yake ni "ku—ku "kuona kwamba." "Yeye aliona kwamba kushutumiwa Kwake Kristo ni mambo makuu kuliko yote Misri ingaliweza kumpa. Misri ilikuwa mikononi mwake. Lakini, hata hivyo, alijua kuifuata njia ya Kristo ilikuwa shutuma, bali alikuwa na furaha sana kujua ya kwamba kulikuwa na kitu fulani ndani yake, kilichomfanya aone njia hii ya Kristo,

kushutumiwa kwa Kristo, hasa, kuwa ni kukuu kuliko anasa zote yeye—yeye alizorithi. Alikuwa na urithi ndani yake uliokuwa mkuu sana kuliko yale urithi wa nje ulikuwa umempa.

42 Loo, laiti tungalikuwa hivyo leo, na kumwacha Roho Mtakatifu atie mafuta hicho kilicho ndani yetu, hiyo imani, kufikia maisha ya kitauwa, yaliyowekwa wakfu kwa Kristo!

Basi, akiwa na imani kama hii aliyokuwa nayo, yeye aliona, na kuhesabu huko kushutumiwa kama heshima.

Leo, mtu fulani anaweza kusema, "Haya, wewe ni mmoja wa wale watu, wale?"

"A-ha, a-ha, vema, a-ha." Mnaona haya kidogo.

Lakini yeye alihesabu hiyo hazina kuu kuliko ulimwengu wote, kwa sababu kulikuwa na kitu fulani ndani yake ambacho angeweza kunena na kusema, "Naam, ni—ninaheshimu hili. Hili linaheshimiwa sana. Nina furaha kuwa mmoja wao." Mnaona? "Nina furaha kujihesabu kama Mwebrania na si Mmisri."

43 Wakristo leo wanapaswa kusema jambo lile lile. "Nina furaha kujihesabu Mkristo, kuacha mambo ya ulimwengu na utaratibu wa ulimwengu. Sio tu kama mfuasi wa kanisa, bali kama Mkristo aliyezaliwa mara ya pili anayeishi kulingana na Maandiko. Ingawa ninaitwa, hata na washiriki wa kanisa, 'mshupavu wa dini,' hata hivyo mimi—mimi—mimi huona hilo kuwa jambo kuu—kuu kuliko vile kama ningekuwa mtu maarufu sana mjini ama katika taifa. Afadhali niwe hivyo kuliko Rais wa Marekani, ama—ama mfalme juu ya nchi. Mnaona? Ni—ninahesabu hiyo kuwa juu zaidi, kwa sababu Mungu katika rehema Zake, kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu—ulimwengu, aliniona, na—na kuweka mbegu ndogo mle ndani, ili kwamba imani yangu iruke juu ya mambo haya ya ulimwengu. Na sasa Yeye ameniita, nami ni—ninajali mahali pangu."

44 Kama vile Paulo alivyosema alihesabu huduma yake kuwa ni kuu sana ... mnaona na loo, kwamba Mungu alikuwa amemwita asije akawa mwalimu mkuu kama Gamalieli, Lakini Paulo alikuwa ameitwa kuwa dhabihu kwa ajili ya Kristo. Mnaona? Sasa jambo lile lile.

Tazama, akiwa na imani kama hiyo hakutegemea kamwe kuona kwake, yale angaliweza kuona. Sasa, hakuona kitu kule isipokuwa kundi la watu wanaoshikashika matope, watumwa, walio kifungoni, wakiuawa kila siku, wakapigwa kwa mijeledi, wakadhihakiwa, imani ya dini yao ilikuwa "ushupavu wa dini." Na kulikuwa na farao ameketi kwenye kiti cha enzi, ambaye hakujua wala kujali chochote kuhusu dini yao. Hakujua kitu kuihusu. Alikuwa kafiri, kwa hiyo yeye ... Ni picha iliyoje ya leo hii. Na hiyo hapo, dini tofauti. Jinsi kwamba kama—kama huyu Musa, akiwa bado kwenye kile kiti pamoja na Rais ama yule mtu mkuu, Farao, kupachukua mahali pale baada ya kifo chake, naye alikuwa mzee. Na hata hivyo Musa alidhani ya kwamba wito huo ... Aliangalia huko nje, na dirisha lile lile ambalo Farao aliangalia nje, maana alikuwa nyumbani kwake.

Naye Farao akatazama nje na kuwaona hao watu waliokuwa wakiinua mikono yao, nao wangechukua mjeledi na kuwapiga hadi kufa kwa sababu walikuwa wakiomba. Wangaliwachoma kwa upanga kwa sababu hata walikosa, kutokutii wakati wo wote, na kuwafanya wafanye kazi hata maskini miili yao ingedhoofika kabisa, na kuwapa chakula haba. "Vema, hawakuwa cho chote ila kundi la washupavu wa dini, hata ni vigumu kuwa wanadamu."

45 Na hata hivyo Musa, imani hiyo ndani yake, iliwaangalia, naye akasema, "Wao ni watu wa Mungu waliobarikiwa." Amina. Ninapenda jambo hilo. Kwa imani kama hiyo, macho yake hayakuangalia uzuri wa Misri, uliangukia kwenye ahadi ya Mungu. Jicho lake la tai na la imani liliona ng'ambo ya hizo anasa za Misri. Yeye, kumbukeni, anakuwa tai sasa. Yeye ni nabii, na jicho lake la tai huinuka juu ya mambo hayo. Loo jinsi ninavyopenda jambo hilo! A-ha! Jamani!

Jinsi mara kwa mara leo, leo, Wakristo hutegemea hisi zao za yale wanayoweza kuona ama yale wanayoweza kufahamu, badala ya imani yao kutegemea yale unayoweza kuyaona kwa jicho lako na anasa. Kama ninyi wanawake, mimi daima huwasihi nikiwaambieni hamna budi kuachilia nywele zenu zikue; haiwapasi kujipaka rangi, hamna budi kutenda kama mabibi na Wakristo. Tazameni barabarani mkawaone wanawake siku hizi wamevalia kizinifu. Vema, unafikiria, "Vema, yeye ni mfuasi wa kanisa; mbona nami siwezi kufanya hivyo?" Mnaona? "Naye anakata nywele zake, mbona—mbona siwezi kufanya hivyo? Vema, yeye anaonekana tu mzuri na mwenye akili, na utu ambao hata mimi mwenyewe sina. Vema, kwa nini siwezi kufanya hivyo? Ninapaswa kufanya hivyo." Unapofanya hivyo, unaipooza imani yako. Mnaona? Hauipi imani yako nafasi ya kustawi. Anzia kwenye jambo hilo, kama nilivyosema.

46 Mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, nchi, watu, wanakuhesabu kama nabii. Haupaswi kuwa ukiwapigia wanawake kelele hivyo, na pia wanaume, juu ya mambo haya. Inakupasa kuwa ukiwafundisha jinsi ya kutoa unabii na kupokea karama.

Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawajui ABC zao?" Mnaona?

Sasa anza tu kutoka kwenye jambo hilo. Jitakaze mwenyewe, ili kwamba unapotembea barabarani uonekane kama Mkristo, kwa vyo vyote, mnaona, na kisha uendelee kutenda kama Mkristo, Mnaona? Na hauwezi kufanya hivyo wewe mwenyewe. Inapaswa Kristo aje ndani yako. Na iwapo hiyo mbegu imo mle ndani, na hiyo Nuru iiguse, itakuwa Hai. Kama haitakuwa Hai, hamna cho chote mle cha kufanywa Hai. Kwa maana, bila shaka imejithibitisha kwa wengine, mnaona, inakuwa hai mara hiyo Nuru inapoigusa.

47 Hilo ni karipio kwa wanawake, najua, wanaosikiza hii kanda ama watakaoisikiza. Ni karipio kwako, dada. Inapaswa kuwa hivyo! Inapaswa kuwa, kwa sababu inaonesha. Sijali umefanya nini; huenda ulikuwa wa kidini, maishani mwako mwote, huenda uliishi kanisani, huenda baba yako ni mhudumu, ama mume wako akawa ni mhudumu; bali mradi tu hutii Neno la—la Mungu, inaonyesha hakuna Uhai mle ndani. Unapooona jambo hilo limefanywa dhahiri, na Uhai wa Roho Mtakatifu, tazama itakapowaguza wengine. Mnaona yale wanayofanya, kama inawaletea. Siyo ajabu ni kwa nini ...

Ni—ni karipio la lililoje kwa wale Mafarisayo, waliomwita Yesu, wakati Yeye angeweza kutambua mawazo yao, wao wakamwita, “Beelzebuli.”

Na maskini yule kahaba akasema, “Mbona, Jamaa huyu ni Masihi. Maandiko yanasema Yeye atafanya haya.” Mnaona, hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu asili ilikuwa mle. Na wakati hiyo Nuru ilipoigusa, ikawa Hai. Hauwezi kuuzuia. Hauwezi kuuficha Uhai.

Unaweza kuchukua na kumwaga saruji juu ya lundo la nyasi, na kuiua katika majira ya baridi kali. Katika majira yajayo ya kuchipua kwa mimea, nyingi ya nyazi zako ziko waapi? Moja kwa moja karibu na ukingo wa zege. Maana hiyo mbegu iliyo tayari kuchipuka chini ya hilo jiwe, wakati jua linapoanza kuangaza, huwezi kuizuia. Itapenyeza njia yake kupitia kule na kujitokeza ukingoni mwake na kuchomoza kichwa chake kwa utukufu wa Mungu. Mnaona, hauwezi kuuficha uhai. Jua linapoguza uhai wa mimea, haina budi kuishi.

48 Na wakati Roho Mtakatifu anapogusa Uhai wa kimaandiko ulio ndani ya mtu, unazaa matunda yake papo hapo. [Ndugu Branham anadata kidole chake — Mh.] Mnaona?

Kwa hiyo haidhuru wewe ni mkweli na mwaminifu iliyoje, unasemaje wewe si mwaminifu, na kunena, akisema walikuwa ... Hawa wanawake wanaovalia hizi—hizi nguo mbaya na kadhalika kule nje, ambao ni wenda uchi wa kupindukia, barabarani; Ingawa hauamini ndivyo ulivyo, hauwezi kujifanya uamini. Unaweza kuthibitisha ya kwamba wewe huna hatia kwa uzinzi, lakini, katika Kitabu cha Mungu, unafanya uzinzi. Yesu alisema, “Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Nawe ulijionesha mwenyewe katika hali hiyo. Mnaona, hauwezi kufahamu hayo isipokuwa Uhai huo umo mle.

Unamtazama mtu mwingine, na kusema, “Vema, namjua Dada Jones. Ndugu Jones ni ... Yeye ni mhudumu. Mkewe hufanya *hivi* na kufanya *vile*.”

Sijali *hilo* linafanya nini; Hili ni Neno. Yesu alisema, “Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli.” Ni Biblia. Na wakati hiyo Nuru inapoigusa, haina budi kuwa Hai. Lazima iwe Hai.

49 Sasa, jicho kuu la Musa, jicho lake la tai, liliangalia zaidi ya uzuri wa Misri.

Mkristo aliye mwamini halisi leo, haidhuru kanisa husema nini, kile mtu ye yote asemacho; hiyo Nuru inapoigusa, wanaona thibitisho halisi la Mungu, hiyo Nguzo ya Moto ikining'inia pale, katika ishara na maajabu yaliyoahidiwa, katika Maandiko yakiwekwa kwake, inakuwa Hai; haidhuru ni ndogo vipi, ama ilivyo chache. Kundi la Mungu daima limekuwa katika uchache. Mnaona? “Msiogope, enyi—kundi dogo, ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa Ufalme.” Mnaona? Wanaipata. Mungu anawajibika kuwapeleka kutoka kila dhehebu, kila utaratibu kila mahali, kuiona, kama wamekusudiwa Uzima.

50 Mtazame maskini Simeoni, aliyekusudiwa Uzima. Wakati Masihi alipokuja hekaluni, katika umbo la mtoto mchanga mikononi mwa mama yake; Simeoni, huko nyuma chumbani mahali fulani, akisoma. Roho Mtakatifu alimwinua, kwa kuwa alikuwa akingojea. Uhai huo ulikuwa ndani yake. Akasema, “Sitaona mauti hata nitakapomwona Kristo wa Bwana.” Na ndiye huyo Kristo wa Bwana hekaluni. Roho Mtakatifu alimtoa kazini mwake na kumwongoza kule naye akampokea huyo mtoto na kusema, “Mruhusu mtumishi Wako, aondoke kwa amani, kwa kuwa macho yangu yanauona wokovu Wako.”

Kulikuwako na mwanamke mzee kipofu pembeni, jina lake Ana, aliyemtumikia Bwana mchana na usiku. Yeye pia alikuwa akitabiri, na kusema, “Masihi yuaja. Ninaweza kumwona akija.” Hata hivyo, yeye alikuwa kipofu. Wakati uo huo, wakati alipokuwa pale ... Huo Uhai mdogo uliokuwa ndani yake uliotabiriwa “Utakuwako! Angekuweko! Angekuweko! Ndipo, Uhai ule ule, ile Nuru ikaja mle jengoni, katika umbo la Mtoto Mchanga, kama “mtoto haramu,” amevikwa nguo Zake za kitoto, akija jengoni. Ndipo Roho Mtakatifu akamgusa yule mwanamke mzee kipofu, naye akaja kwa Roho, akaongozwa kupitia kwa watu, na akasimama juu ya Mtoto huyu mchanga; na akambariki mama huyo na kumbariki Mtoto huyo mchanga, na kumwambia yale yangekuwa wakati ujao Wake. Mnaona, walikusudiwa Uzima! Mnaona?

Waangalie, hapakuwa na dazani yao. Kulikuwako na watu wanane tu waliookolewa katika siku za Nuhu, si wengi sana, bali wote waliokusudiwa Uzima waliingia wakati huo. Angalia jinsi Roho Mtakatifu anavyotenda kazi katika kila wakati, akiwavuta watu.

51 Sasa tunaona ya kwamba imani ya Musa ilimwongoza kuangalia kile kitakachokuwa, si kile kilichokuwa. Angalia kesho badala ya leo. Angalia ahadi badala ya anasa. Waangalie watu badala ya madhehebu. Mnaona? Mungu alifanya hivyo.

Lutu angeweza kuona anasa za ufanisi huko Misri, ama kule Sodoma. Lutu alingeona uwezekano wa—wa ... wa pesa nyingi sana. Lutu aliweza kuona ninii ... uwezekano alipotazama kule Sodoma na labda angekuwa... Kwa kuwa alikuwa Mwebrania, huenda akawa mtu mkuu kule, kwa maana alikuwa mtu mwenye akili sana, na mpwake Ibrahimu, kwa hivyo akachagua kuelekea Sodoma. Akili za Lutu zilimwongoza kuona anasa za—za ufanisi. Akili za Lutu zilimwongoza kuona baraka za—za anasa. Lakini, imani yake ilipoozwa sana nazo, hakuona moto ambao ulikuwa ukienda kuangamiza maisha kama hayo.

Na hivyo ndivyo watu walivyo siku hizi. Wanaona uwezekano wa kuwa wafuasi wa dhehebu kubwa, wanaona uwezekano wa kuwa na hadhi ya kijamii na watu wa mjini, lakini hawaoni uwezekano wa ... Hawaoni imani yao imepooza. Hebu nirudie hayo kusudi isieleweke vibaya. Wanawake leo, kama nisemavyo, wanataka ku—wanataka kutenda kama wachezaji mashuhuri wa sinema. Watu leo wanataka kutenda kama wachekechaji wa televisheni.

52 Wahubiri siku hizi yaonekana wanataka kuyafanya makanisa yao kama loji za kisasa za aina fulani, uanachama na kadhalika. Wanaona uwezekano wa labda kuwa askofu ama msimamizi mkuu, ama kitu kama hicho, kama wataambatana na kanisa; tukiyaacha Maandiko, yanapokuwa moja kwa moja mbele zao, yakithibitishwa kabisa na Nguvu za Mungu, na kwa Neno la Mungu lililo hai likiishi ndani ya watu. Hata hivyo, hawalitaki. Wanasema, "Hatutaki kuchanganyikana na kitu kama Hicho." Ingeondoa kandi yao ya ushirika. Ingeondoa taratibu zao za kidhehebu. Hata hivyo mtu mwaminifu, kama Lutu, akiketi chini Sodoma, akijua ya kwamba hilo ni kosa. Mnaona? Mnaona? Wanafanya nini wanapofanya hivyo? Wanaipooza imani yao ndogo waliyokuwa nayo. Haiwezi kufanya kazi.

53 Sasa, Musa aliachilia jambo hilo, akaelekeza imani yake ... akaupooza ulimwengu.

Ama imani yako itapooza anasa, ama anasa zitapooza imani yako. Naam, huna budi kuchukua moja au nyingine. Na mnaona Biblia haibadiliki. Mungu habadiliki. Yeye ni Mungu asiyebadilika.

Na sasa tunaona, leo, ya kwamba watu wa siku hizi, mnaona, wanaangalia mambo makubwa, madhehebu makubwa. "Mimi ni mfuasi wa *Fulani*." Mnaona? Nao wanashuka kwenda kule, na, angalia, hakuna tofauti na watu wa mitaani. Hakuna mambo mengine. Wana kitu kidogo cha kiakili, na kuendelea. Unapozungumza juu ya uponyaji wa Kiungu, Nguzo ya Moto, Nuru ya Mungu, wao husema, "Hilo ni la akili."

54 Mtu fulani alichukua picha ya Malaika wa Bwana, hivi majuzi, mhudumu wa Kibatisti, na kuicheka. Mnaona, hiyo—hiyo ni kukufuru. Mnaona? Hakuna msamaha kwa hilo.

Hivyo ndivyo Yesu alivyosema, mnaona. Ni kukufuru; unapoiona ikifanya kazi zile zile alizofanya Kristo. Naye akasema ... Wakati walipoona hizo kazi katika Kristo, Yeye alikuwa dhabihu, nao wakamwita "Beelizebuli," ibilisi," kwa sababu alikuwa akifanya hivyo. Na sasa wanasema ... Yeye alisema, "Nawasamehe hayo. Bali Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, ukinena neno moja dhidi Yake, hautasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao." Mnaona? Neno moja tu ndilo unalopaswa kusema dhidi Yake. Mnaona? Na halafu ...

Kwa sababu, kama Uhai huo, iwapo umekusudiwa Uzima wa Milele, basi huo Uhai utabubujika utakapoiona. Ungeitambua, kama maskini yule mwanamke kisimani, na—na watu mbalimbali. Lakini iwapo haimo mle, haiwezi kuwa Hai kwa kuwa hamna cha kuifanya Hai. Kama alivyozea kusema maskini mama yangu, "Hauwezi kupata damu kutoka mboga nyekundu," kwa maana hamna damu mle. Sasa, hilo ni jambo lile lile.

55 Na linapooza imani ndogo uliyo nayo. Lutu angeona zile anasa, bali hakuwa na imani ya kutosha kuona ule moto ambao ungeangamiza anasa kama hizo.

Nashangaa kama tunayo leo? Nashangaa kama sisi, vema, kama wanawake wanaotaka kupendwa na watu wote, wanaotaka kutenda kama wa—wanawake wengine kanisani, kama kama wakiona ya kwamba wanataka ku—kutenda kama wengine. Wao—wao wanaweza kuona uwezekano wa kuwa m—m—mwanamke mrembo zaidi, kwa kupakwa rangi. Wanaweza kuona mwanamke mrembo zaidi kwa kuwa na umbo la ujana, kwa kukata nywele zao na kutenda kama wengine wa wachezaji mashuhuri wa sinema, Lakini nashangaa kama hilo halijapooza imani yao, kujua ya kwamba Biblia inasema ya kwamba, "mwanamke anayefanya jambo hilo ni ninii- ... mwanamke asiye na heshima," na, "Na mwanamke anayevalia mavazi yanayompasa mwanamume , ni chukizo mbele za Mungu," suruali ndefu na kadhalika, na suruali fupi wanazozivalia. Na—na imekuwa ukatili hivi kwamba hata limekuwa jambo la kawaida kwa

watu wanaofanya hivyo. Nashangaa iwapo hao hawaipoozi ile imani haba kabisa waliyokuwa nayo hata kwenda kanisani, mnaona. Hilo ndilo jambo ilifanyalo.

56 Lutu alifanya hivyo, na ikampooza na kuwapooza watu wake kule chini. Hawangaliiona,

Bali Ibrahimu akiwa na imani iliyothibitishwa, mjomba wake, hakutazama zile anasa, hakutaka uhusiano wo wote nazo, ingawa ilimlazimu kuishi maisha magumu na kujiishia mwenyewe. Na Sara akaishi kule jangwani ambako alipata shida, katika nchi yenye ukame. Lakini hao hawakutazama zile anasa wala uwezekano wa kupendwa na watu.

Sara, mwanamke mrembo sana nchini, Biblia ilisema hivyo. Alikuwa mzuri, aliye mzuri sana katika wanawake. Na sasa yeye hata alikaa na kumtii mumewe, hata yeye alimwita "bwana" wake, ambaye Biblia humtaja hata katika—katika Agano Jipya ikasema, "Nanyi ni binti zake mradi tu mnatii ile imani." Mnaona, alimwita mumewe "bwana" wake.

Naye Malaika wa Bwana akazuru hekalu ... ama hema yao ndogo kule, na akawaambia. Hata hawakuwa na nyumba ya kuishi; wakiishi huko katika nchi ya jnagwa. Na hivyo ndivyo ilivyo. Mnaona siku hii imefananishwa tena, kabisa na ilivyokuwa wakati huo?

57 Sasa, Musa kwa imani yake kuu tena angesema kusema, "La" kwa mambo ya kisasa ya ulimwengu wa kisasa, na kufanya chaguo lenye haki. Alichagua kupata mateso pamoja na watu wa Mungu. Alichagua kwenda nayo. Kwa nini? Imani yake! Aliona ahadi. Aliona wakati wa mwisho. Aliona hata ya kesho, na akaachilia imani yake. Naye hakujali yale macho yake yaliyoona katika uwezekano hapa kwamba yeye alikuwa farao naye angekuwa farao. Yeye alitazama hata akaona ya kesho.

Loo, laiti watu wanalifanya hivyo, hakuona ulimwengu wa sasa. Kama ukiutazama ulimwengu wa sasa, utauchagua. Yafiche macho yako toka kwake, ukatazame ahadi ya Mungu, kule mbali katika mambo ya kesho.

Kwa imani yake yeye angechagua. Alichagua kuitwa mwana wa Ibrahimu, na akakataa kuitwa mwana wa Farao. Angewezaje hivyo, huku katika ufalme wote ... Misri ilikuwa imeshinda ulimwengu. Yeye alikuwa mfalme wa ulimwengu, akiwa kijana wa miaka arobaini, hapa tayari kutawazwa. Lakini kamwe hakuangalia ninii yake ...

58 Tazama wanawake ambao wanalikuwa karibu naye siku kwa siku, wengi mno. Tazama hizo anasa, kuketi na kunywa divai na kutazama michezo ya kuvua nguo zao mbele yake huku wakicheza na kumpepea hewa kwa ... Na wanawake kutoka ulimwenguni kote, na vito na hazina na jeshi lake nje kule. Alichopaswa kufanya tu ni kuketi kitako na kula chakula chake kitamu na kusema, "Tuma nini ... tuma jeshi kikosi nambari *fulani* humu kufanya *hivi na vile*; teka taifa hilo. Ninaamini ninalitaka." Hivyo tu ndivyo alivyopaswa kufanya. Kuketi mle, nao wampepee hewa, na kuufungua mdomo wake, ndiposa wale—wale warembo, wenda uchi wa siku hizo, wamwage divai kinywani mwake, wamlishe chakula chake huku wamemkumbatia kwa mikono yao, wanawake wote walio warembo sana ulimwenguni. Anasa zote zilizokuwemo, zilikuwa papo hapo karibu naye.

Bali yeye alifanyaje? Alitazama mbali na hayo. Alijua moto ulikuwa tayari kwa hayo. Yeye alijua mauti yalikuwa katika mstari huo. Mnaona? Alijua ilikuwa hivyo. Naye akatazama kwenye kundi la watu waliodhihakiwa na kukataliwa, na kwa imani yeye akachagua kupata shutuma za Kristo na akajiita mwenyewe, "Mimi ni mwana wa Ibrahimu. Mimi si mwana wa huyu farao. Ingawa unanifanya askofu, ama shemasi, ama askofu mkuu, ama papa, mimi si mwana wa kitu hiki. Mimi ni mwana wa Ibrahimu, na ninajitenga na mambo ya ulimwengu." Amina, amina, na amina! Kwa imani, alifanya hivyo!

59 Akaondosha hizo anasa. Akaondosha uwezekano wa kuwa halifa wa askofu, akaondosha u—uwezekano wa kuwa halifa wa askofu mkuu ama mwangalizi mkuu katika uchaguzi ujao ama cho chote kile, akaondolea hayo mbali. Akakataa kuyaangalia.

"Sasa, kama nikiwa askofu, nitaingia na watu watasema, 'Baba Mtakatifu,' ama-ama 'Daktari Fulani,' ama-au-au-au 'Mzee Fulani-na-fulani.' Jinsi watakvayofanya, wahudumu wote mkutanoni, watanipigapiga mgongoni, na kusema, 'Aisee, jamani, jamaa huyo ana kitu fulani, ninawaambieni. Loo, sh-sh-sh, tulieni, huyu hapa askofu anakuja, mnaona. Asemayo, hayo ndiyo sheria. Mnaona, huyu hapa anakuja *Fulani*.'" Watu wataruka kwa ndege ulimwengu mzima kuwa...kumwona papa, wambusu mguuni na pete na kadhalika. Ni uwezekano ulioje kwa Wakatoliki, ni uwezekano ulioje kwa Waprotestanti, kuwa askofu ama msimamizi mkuu, ama cho chote kile, mtu mkubwa katika dhehebu lao.

Kutazama, hata hivyo, lakini mnaona jicho la imani huangalia mbele ya hayo. Nanyi mnaona mwisho wake kule chini, ambapo, Mungu anasema kitu hicho chote kitaangamizwa. Imani, hilo jicho la tai, linakuinua juu ya haya nawe unaona ya kesho, si ya leo, na kuchagua kuitwa mwana wa Ibrahimu.

60 Farao kwa kutokuwa na imani aliwaona watoto wa Mungu kama washupavu wa dini. Bila imani, aliwafanya watumwa kwa sababu hakuogopa aliyosema. Yeye hakumwogopa Mungu. Alidhani ya kwamba

yeye alikuwa ni mungu. Yeye alifikiri mi—miungu yake aliyoitumikia, ya kwamba alikuwa askofu, yeye alikuwa msimamizi mkuu, miungu yake ndiyo iliyofanya jambo hilo. “Hamna chochote kwa jambo hili hapa, kwa hivyo akawafanya watumwa. Aliwacheka, akawadhihaki. Kama tu vile watu walivyofanya siku hizi, jambo lile lile hasa.

Imani ya Musa iliwaona katika nchi ya ahadi, watu waliobarikiwa. Huenda ikawa ni vita vikali kuwapeleka kwenye ahadi, lakini Musa alichagua kwenda pamoja nao. Jinsi ambavyo ningeweza kukaa juu ya jambo hilo, bali wakati wangu unakwisha. Mnaona?

61 Tazama, huenda ikawa jambo gumu kuwabadilisha watu hao. “Huna budi kwenda kuishi nao, huna budi kuwa mmoja wao, nao tayari wana akili sana hata hauwezi kuwatikisa. Mnaona? Lakini hapana budi jambo fulani litendeke kule. Hapana budi ya kimbinguni yaoneshwe mbele zao. Litakuwa ni jambo gumu. Madhehebu yatakukataa, na mambo haya yote yatatukia. I—itakubidi kufanya mambo ya kutisha, hata hivyo, fanya chaguo lako.”

“Mimi ni mmoja wao.” Naam. Imani yake ilifanya hivyo. Imani yake ikatoa spaki. Naam, bwana. Yeye aliiona. Lilikuwa jambo gumu kuwapeleka kwenye hiyo ahadi, bali akafanya chaguo lake kwenda pamoja nao kwa vyo vyote. Bila kujali walimfanyia nini, jinsi walivyomkataa, alienda kwa vyo vyote. Naye alitoka pamoja nao.

Sasa natumaini mnasoma. Vema. Nenda pamoja nao, hata hivyo. Fanya, uwe mmoja wao, hiyo ni kweli, kwa sababu ni wajibu wako. Labda mna vita vikali, na mambo mengi utakayopitia, bali nenda kwa vyo vyote.

62 Bali imani yake ilimwongoza kuchukua chaguo la Neno, na siyo anasa. Alichukua Neno. Hivyo ndivyo imani ya Musa ilivyofanya. Wakati imani inapotazama walio wabaya sana wa Mungu ... kumbukeni, hapa ilikuwa ile anasa sasa, ulimwengu, aliye wa juu sana, mfalme wa ulimwengu. Na ahadi ya Mungu ilikuwa wapi? Kwenye shimo la matope, wakanyaga matope.

Lakini wakati imani, wakati imani inapoangalia walio wabaya sana wa Mungu, inawahesabu kuwa wa kuu sana na wenye dhamani kuliko yale bora sana ulimwengu uwezayo kuonesha. Naam, bwana. Wakati imani inapoliangalia, wakati imani inapoweza kuliona, wakati imani katika Neno inaweza kuona Neno likidhihirishwa, ni zaidi ya anasa zote na uaskofu mkuu na kila kitu unachoweza kunena. Imani hufanya hivyo. Mnaona? Unaweza kuwaona walio wabaya sana, wanaodharauliwa, waliokataliwa, na cho chote kile; na wawe wabaya vipi, hata hivyo imani itawahesabu hao kuwa maili milioni moja juu sana kuliko yaliyo bora sana ulimwengu unayoweza kufanya. Amina! Hivyo ndivyo tunavyoimba ule wimbo, “Nitaiendea njia ya watu wachache wa Bwana wanaodharauliwa.” Mnaona? Loo, jamani!

63 Kwa kuwa, mnaona, imani huona yale Mungu anayotaka yafanywe. Loo, natumaini hili litaingia. Imani haiangalii wakati wa sasa. Imani haioni jambo hili hapa. Imani hutazama kuona kile Mungu anachotaka, na inafanya kazi ipasavyo. Hivyo ndivyo imani inavyofanya. Inaona yale Mungu anayotaka, na yale Mungu anayotaka yatendeke, na imani hutenda kazi kupitia jambo hilo.

Imani ni ono la mbali. Haifupishi upeo wake. Hushikilia ionacho. Amina! Mpiga risasi yeyote mzuri anajua hilo. Mnaona? Hiyo, hulenga mbali. Ni—ni darubini. ni darubini kubwa, ni darubini ya macho ambayo haioni *hapa* karibu; Hutumii darubini ya macho kutazama ni saa ngapi, mnaona, huitumii hiyo. Bali hutumia darubini ya macho kutazama mbali kabisa.

Na imani hufanya hivyo. Imani huitwaa darubini ya macho ya Mungu, zote mbili, pande zote mbili, Agano Jipya na Agano la Kale, na kuona kila ahadi aliyoifanya. Nayo imani huiona kule ng'ambo, na imani huchagua hiyo, bila kujali wakati uliopo usemavyo *hapa*. Yeye hutazama kule mwisho. Yeye hashushi darubini yake na kutazama upande *huu*. Hutazama kule ng'ambo. Yeye huweka kipini cha kulengea shabaha katikati ya Neno kabisa. Hivyo ndivyo imani ifanyavyo. Hiyo ni imani iliyo ndani ya mtu inayofanya mambo hayo.

64 Sasa tazama. Yale Farao aliyoita, ya wito, yale Farao aliyaita makuu, Mungu aliyaita “chukizo!” Farao angeweza kusema, “Angalia, Musa, hapa, mbona, wewe ni farao anayefuata. Ni—nitakukabidhi fimbo hii ya ufalme ninapoondoka hapa. Nitakupa fimbo hii. Ni yako. Mnaona? Sasa, hili ni kuu. Utakuwa mtu mashuhuri, Musa. Utakuwa askofu. Utakuwa *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*. Usituache. Wewe kaa hapa.” Lakini mnaona, yeye aliita hayo mambo *makuu* naye Mungu akayaita *machukizo*.

Sasa, ninyi wanawake fikirieni kwa dakika moja, kwa hiyo, ninyi wanaume. Kile ulimwengu unachoita *kikuu*, Mungu anakiita “*uchafu*.” Je! Biblia haisemi, “Ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi linalompasa mwanamume”? Nawe unafikiri wewe ni mwerevu katika kufanya jambo hilo. Mnaona? Wewe unaonesha tu mwili wa kike kwa ajili ya ibilisi, na hivyo tu. Kwa hiyo, usifanye hivyo.

Ewe wanamume mnaoishia mambo ya ulimwengu, na kushika na kukumbatia haya! Nanyi wanaume ambao hamna ujasiri wa kutosha kuwafanya wake zenu na kadhalika kuacha kufanya jambo hilo, aibu kwenu! Nawe unajiita wana wa Mungu? Inaonekana kama usodoma kwangu. Mnaona? Si kwa ajili ya

kuwaudhi, bali kuwaambia Kweli. Upendo husahihisha. Daima ndivyo ilivyo. Mama ambaye hawezi kumtuza mtoto wake, amkamsahihisha, na kumchapa, na kumfanya awe na tabia nzuri, yeye si mama kutosha. Hiyo ni kweli.

65 Sasa, na angalia kile kinachotukia sasa. Musa aliona jambo hili, kwa ono lake. Naye Farao akasema ya kwamba, “*Hili ni kuu.*” Mungu alisema, “Ni chukizo.” Kwa hiyo Mungu ... Musa alichagua yale Mungu aliyosema.

Sasa, angalia, imani huona yale Mungu anayotaka uone. Mnaona? Imani huona yale Mungu anayoona.

Na hoja na hisi zinaona kile ulimwengu unachotaka uone. Angalia hoja, “Mbona, ni akili ya kibinadamu tu. Ni—ni sababu tu ya kwamba hii ... Vema, *hii* si ni nzuri tu?” Mnaona? Hiyo ni kweli kabisa, unapotumia hizo hisi ambazo ni kinyume na Neno, mnaona, basi hilo ndilo ulimwengu unalotaka uone.

Lakini imani haiangalii jambo hilo. Imani huangalia yale Mungu aliyosema. Mnaona? Mnajua, mnatoa hoja.

66 Sababu, hoja, huona kile ulimwengu unachotaka uone, madhehebu makubwa. Vema, wewe ni Mkristo? “Loo, mimi—mimi ni Mpresbiteri, Mmethodisti, Mluteri, na Mpentekoste, kadhalika. Mimi ni *hiki, kile*, ama *kinginecho.*” Mnaona, *hiyo, hiyo* ni hisi. “Mimi ni mfuasi wa kanisa la kwanza, mnaona. Loo, mimi ni Mkatoliki. Mimi ni—mimi ni *huyu, yule.*” Mnaona, unasema hivyo. Sasa, hizo, hizo ni hisi. Unapenda kusema hivyo kwa sababu ni dhehebu, kitu kikubwa. “Vema, tu—tu—tuna washiriki wengi, karibu, kuliko kanisa lolote ulimwenguni, mnaona. Sisi ...”

Lakini kuna Kanisa moja tu halisi, wala hujiungi nalo. Unazaliwa ndani Yake. Mnaona? Na kama umezaliwa ndani Yake, Mungu Aliye Hai hutenda kazi kwako, na kujitambulisha Mwenyewe. Mnaona? Hapo ndipo Mungu anapoishi, katika Kanisa Lake. Mungu huenda Kanisani kila siku, anaishi tu Kanisani. Yeye anaishi ndani yako. Wewe ni Kanisa Lake. Wewe ni Kanisa Lake. Ninyi ni Maskani anayoishi Mungu. Wewe ni Kanisa la Mungu aliye hai, wewe mwenyewe. Na kama Mungu aliye hai anaishi katika kiumbe Chake kilicho hai, basi matendo yako ni ya Mungu; kama sivyo, basi Mungu hayuko mle ndani. Yeye asingekufanya utende hivyo, wakati anaposema katika Neno hapa, ramani Yake, “Usifanye hivyo,” nawe unafanya. Mnaona, hilo ni kosa. Unapokana hilo, basi hiyo inaonesha ya kwamba Uzima huo hata haumo ndani yako. Mnaona? Hiyo ni kweli.

67 Imani ilimwongoza Musa kwenye njia ya utii. Angalia, Musa alifanya ... Hapo kuna Farao kijana, hapo kuna kijana Musa, wote wawili wakiwa na nafasi. Musa aliona kule kushutumiwa kwa hao watu, na akakuhesabu kuwa hazina kuu kuliko yote Misri iliyokuwa nayo. Naye, akiongozwa na imani, alifuata yale imani yake ilisema katika Neno, nayo ikamwongoza kwenye njia ya utii, na hatimaye akaingia Utukufuni, asiyekufa, asife kamwe, Mbele za Mungu. Kuona na hisi, zilimwelekeza, na anasa, zilimwongoza Farao kwenye kifo chake na maangamizi ya Misri, taifa lake na halijainuka tena tangu wakati huo.

68 Haya basi. ukitazama *hili*, utakufa. Ukitazama *Kile*, utaishi. Sasa fanya chaguo lako. Hilo ndilo jambo lile lile Mungu aliloweka mbele ya Adamu na Hawa, katika Bustani ya Edeni. Mnaona? Kwa imani, huna budi kufanya chaguo lako.

Sasa tazama, kuona kulimwongoza Farao mautini, na kwenye maangamizi ya jiji lake.

Musa, kwa imani yake, kamwe hakumwogopa Farao. Mnaona? Yeye hakujali yale Farao aliyosema. Hakujali kuhusu Farao, si zaidi ya vile mama yake na baba yake walivyojali vitisho vyao. Wakati Musa alipothibitishiwa kuwa ndiye, naye alikuwa mtu atakayeikomboa Misri ... ama kuwaongoza Israeli kutoka Misri, hakujali aliyosema Farao. Yeye hakumwogopa. Amina, amina, amina! Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.]

Hakuna hofu katika imani. Imani inajua jambo hilo. Imani, kama nilivyosema daima, ina misuli mikubwa mno, na nywele kifurani. Imani husema, “Nyamaza!” na kila mtu hunyamaza. Hivyo tu. “Ninajua mahali nilipo!”

Wengine wao husema, “Vema, labda yeye yu ajua.” Mnaona?

Lakini huna budi kusimama na kuonesha misuli yako. Hivyo tu. Imani hufanya hivyo.

69 Angalia, Musa hakumwogopa Farao baada ya Mungu kuthibitisha wito wake. Wakati Musa alipoamini alitwa kwa ajili ya jambo hilo, lakini wakati Mungu alipomwambia kule juu, “Ndivyo ilivyo,” naye akashuka na kuonyesha mbele ya Farao na wengine wote ya kwamba alitumwa kufanya hivyo, Musa hakumwogopa Farao kamwe.

Angalia, Farao alitumia hekima yake juu ya Musa, hata hivyo. Tazama. Akasema, “Nitakwambia nini, ni—nitafanya mapatano nawe.” Baada ya mapigo kumla, alisema, “Nitafanya mapatano na wewe. Nendeni

tu kwa ushirika mdogo, wa siku tatu. Nendeni tu umbali fulani, na msiende mbali zaidi." Lakini, mnajua, ninii ... Hayo yalikuwa yale hisi za Farao ziliyomwambia, mnaona, "Nendeni umbali fulani lakini msiende mbali zaidi."

Je, hatuna watu wa namna hiyo siku hizi? "Kama ukijiunga na kanisa, hiyo ni sawa."

70 Lakini, mnajua, imani aliyokuwa nayo Musa haikuamini katika "dini ya umbali fulani." Akasema, "Sote tutaenda. Tutaenda kabisa. Hiyo ni kweli. Tunaenda kwenye nchi ya ahadi. Hatuondoki kwenda hapa nje tukajiundie dhehebu, na kukoma hapo. Tutaendelea mbele kabisa." Amina. "Ninaenda kwenye nchi ya ahadi. Mungu alituhidi."

Ni Mafarao wangapi tulio nao leo wamesimama mimbarani, wakuu wa madhehebu! "Sasa, kama ukifanya tu *hivi* na kufanya *vile*, hivyo tu. Vema, mnaona, mbali tu."

Lakini Musa alisema, "Loo, la! La, la! La, la!" Mnaona?

Farao akasema, "Vema, mbona? Kama mtakuwa na dini ya namna hiyo, nitawaambia la kufanya, wewe tu na wazee nendeni mkaabudu, mnaona. Wewe tu na wazee nendeni mkaabudu. Kwa sababu, nyote mnaweza kuwa na dini ya namna hiyo, lakini msieneze miongoni mwa watu."

71 Mnajua yale Musa aliyosema? "Hamna hata ukwato utakaoachwa nyuma. Tutaenda kabisa. Tutaenda sisi sote! Siendi kama wao hawaendi. Na, mradi tu niko hapa, nimo mikononi mwako." Amina. "Siendi isipokuwa wao waende pia, na hivyo tu." Loo, ni mtumishi hodari iliyoje! Amina. "Nataka kuwachukua pamoja nami. Kwa sababu tu nimeipata, nami naketi kitako na kusema, 'Vema, *hii* ni sawa'? La, bwana. Tunataka hao watu, pia. Kila mmoja wetu anaenda." Amina. Yeye akasema, "Nasi hatutaacha hata mmoja wa kondoo wetu wala chochote, nyuma. Hakuna kwato itakayoachwa nyuma. Sote tunaenda kwenye nchi ya ahadi." Amina!

"Kila mmoja wetu! Hata kama wewe ni mke wa nyumbani, ama ni—ni yaya mdogo, ama hata kama wewe ni mwanamke mzee, ama kijana mwanamume, ama cho chote kile, tutaenda, kwa vyo vyote. Hakutakuwa na mmoja wetu atakayesalia." Amina. "Kila mmoja wetu ataenda, hatutazuiwa na kingine chochote." Hiyo ni kweli. Jamani! Hizo dini kweli zilikuwa katika mjadala moto moto kule, sivyo? Loo, jamani!

Hasha, Musa hakuamini katika hii "dini ya umbali fulani tu." La, hakuamini jambo hilo. A-ha. Naam, bwana. Loo, jamani!

Tungeweza kukaa siku nzima kwenye jambo hilo, bali sina budi kulifikia somo langu baada ya kitambo kidogo na kuanza kuhubiri.

72 Angalia, angalia jambo hili, jinsi lilivyo zuri! Loo, napenda jambo hili. Mnajua, hatimaye, Farao alisema, "Ondokeni!" Mungu alimpiga tu, kwa sauti ya Musa. Alipiga kila kitu. Yeye alifanya kila kitu kilichopaswa kufanywa. Akakomesha ninii...akalifanya jua litue mchana katikati. Yeye alifanya kila kitu kingine. Yeye—akautia mchana giza. Akawaleta vyura, viroboto, chawa, kila kitu; moto, moshi na mauti kwa familia zake, na kadhalika. Yeye alifanya kila kitu mpaka, hatimaye, ilimbidi Farao kusema, "Ondokeni! Chukueni yote mliyo nayo, mwondoke." Loo, jamani! Sifa ziwe kwa Mungu!

Nina furaha sana kwamba mtu anaweza kumtumikia Mungu kabisa hata yeye, Ibilisi, hajui la kufanya naye. Hiyo ni kweli. Alimtii Mungu kabisa kabisa hata ibilisi akasema, "Loo, jamani, ondokeni! Si—sitaki kusikia hayo tena." Hiyo ni kweli. Unaweza kufanya hivyo, kabisa.

73 Mnaona sasa, kama—kama Mungu hangalimuunga mkono Musa, basi angalikuwa mtu wa kuchekwa. Lakini Mungu alikuwa papo hapo, akithibitisha. Kila kitu alichosema, kilitimia.

Naye Farao ilimbidi kushikilia wadhifa wake, maana alikuwa askofu, mwajua, kwa hiyo a—ilimbidi kukaa pale. Asingeweza kukana. Asingeweza kusema hapana, kwa sababu tayari ilikuwa inatendeka. Mnaona? Hangeweza—hangeweza kuikana, kwa sababu ilikuwa tayari inatendeka. Kwa hiyo hatimaye akasema, "Loo, ondokeni tu! Sitaki kuwasikia tena. Ondokeni hapa! Chukua yote uliyo nayo, na ondokeni!" Loo, jamani!

74 Sasa tunaona Musa, hapa, baada ya Mungu kumfanyia mengi, na kumwonesha ishara nyingi sana na maajabu. Sasa, kwa dakika kumi na tano zifuatazo, hebu tuweke hili hapa chini. Na angalieni kwa makini sana. Musa alikuja mahali hapa ambapo yeye ...

Mungu alikuwa amesema, "Niko pamoja nawe. Maneno yako ni Neno Langu. Nimekuthibitishia hilo, Musa. Wewe, wakati hakukuwa na nzi nchini, haukuwa wakati wake, nawe ukasema, 'Na waje nzi,' na nzi wakaja." Huo ni uumbaji. Ni nani awezaye kuleta giza juu ya nchi, ila Mungu? Yeye alisema, "'Iwe giza, 'na kukawa na giza. Ulisema, 'Na kuwe na vyura,'" na wale vyura hata wakaingia katika nyumba ya Farao, vitandani, nao walipolundikana katika mafungu makubwa. Muumba! "Nami nimenena kupitia kwako, Musa, na—na kulifanya Neno Langu liumbe kupitia midomo yako. Nimekufanya kuwa mungu mbele ya

Farao." Naam, bwana. "Nimefanya haya yote."

Na hapa wakafikia mahali, kesi ndogo ikatokea, na Musa akaanza kulia, "Nifanye nini?"

75 Ninawatakeni mwone. Hili ni somo kuu hapa sasa. Ninapenda jambo hili, mnaona. Mnaona, Musa, kama tukisoma hapa vizuri, ya kwamba Mo- ... Wakati, hao wana walipoanza kuogopa, walimwona Farao akija, akiwa kazini.

Mungu alikuwa amefanya kila kitu kikamilifu. Sasa Yeye aliwatia safarini. Yeye amelikusanya kanisa pamoja. Walikuwa tayari wameitwa watoke. Wanatoka katika kila dhehebu. Wote walikusanyika pamoja. Musa akarudi kule nyuma na kusema, "Bwana, nifanye nini?"

Angesema, "Vema, nenda ukafanye *hivi*." Vema, endelea. "Sasa, Musa, unajua nimekuita kufanya jambo hili."

"Naam, Bwana."

"Vema, nenda ukazungumze *hili*, na itakuwa," hawa hapa inzi wakaja. "Nena kwa ajili ya *hili*," na hili hapa. "Fanya *hili*," hili hapa. Kila kitu kilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI, BWANA ASEMA HIVI, BWANA ASEMA HIVI! Sasa anaingia katika shida ...

76 Ndipo Mungu akasema, "Basi, wameanza safari yao. Wote wameitwa watoke. Kanisa liko pamoja, kwa hivyo nimewaweka safarini. Basi, Musa, waongoze huko. Nalikwambia la kufanya. Nitaketi chini na kupumzika kidogo."

Musa alisema, "Ee Bwana, angalia wanakuja, huyu hapa Farao anakuja! Watu wote ... Nifanye nini? Nifanye nini?" Angalia pale, si huo ni uanadamu tu. Naam, bwana. Akaanza kulia, "Nifanye nini?"

Hapa tunamwona Musa akidhihirisha, asili ya kibinadamu kikamilifu, kila mara unataka Mungu aje nyuma yako na kukusukumiza kwenye jambo fulani. Sasa, hiyo sisi leo hii. Unataka Mungu, baada ya sisi kuona yote ambayo tumeona, hata hivyo unataka Mungu akusukume ufanye jambo fulani. Mnaona?

Musa alikuwa tayari amekuwa mzembe, kasema, "Mungu, nitakuuliza, nione utasemaje. Naam, naam, unasema hivyo. Vema, vema, nitasema, pia." Mnaona?

Lakini hapa Mungu alikuwa amemchagua kwa ajili ya kazi hiyo, akathibitisha ya kwamba alikuwa pamoja naye. Na huyu hapa, hali inakuja, ndipo anaanza kulia, "Nifanye nini? Bwana, nifanye nini?"

77 Sasa mnakumbuka, yeye alikuwa tayari ametabiri hapa, kwa kuwa alisema, "Hawa Wamisri mnaowaona leo, hamtawaona tena." Na ndipo mara moja akaanza kupaza sauti, "Mungu, tufanyeje?" Mnaona? Baada ya yeye kufanya kazi nzuri sana katika kutabiri pale. Unaona, yeye aliwaambia tayari jambo ambalo lingetukia. Kama Neno la Mungu lilikuwa ndani yake, lilikuwa ndani yake. Na wakati alipokuwa akisema jambo hilo, kwa kweli lilitimia. Yale aliyosema yalikuwa tayari yanaenda kutimia, na hapa alikuwa akilia, "Nitafanya nini?"

Loo, kama huo si ubinadamu! Kama huyo si mimi! Kama huyo si mimi! Mnaona?

Alikuwa tayari amethibitisha, "Yale usemayo yatatukia. Niko pamoja nawe."

Na hapa hali ikatokea katika dakika moja. "Nifanye nini? Nifanye nini, Bwana? Ee, Bwana, uko wapi? Ee, unanisikia? Nifanye nini?" Naye alikuwa tayari amemchagua, na kumthibitisha, na kumhakikisha na kufanya kila kitu kupitia kwake. Na hapa, "Mungu?" Loo, jamani! Akielezea kikamilifu, mwanadamu hupenda kustarehe na kumwacha Mungu amsukume.

78 Na, hata hivyo, alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemtia mafuta kwa ajili ya kazi hii, kufanya jambo hili, na Mungu alikuwa amethibitisha dhahiri madai yake. Ulikuwa ni wakati wa watu kukombolewa. Mungu, kupitia miujiza yake na maajabu, alikuwa amewavuta wote pamoja katika kundi moja. Mnanifuata? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Akawaleta wote pamoja katika kundi moja, akathibitisha madai yake. Maandiko yalisema hivyo; hii hapa ishara, huu hapa ushahidi hapa, kila kitu alichosema. Ndipo akaja miongoni mwao kama nabii. Daima, cho chote alichosema, Mungu alikitimiza, hata kuumba na kuwaleta inzi, na kufanya vitu viweko. Na kila kitu alichokuwa amemwahidia, hapa akakifanya.

Lakini yeye alitaka kungojea BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Alipaswa kujua ya kwamba thibitisho lenyewe la wito wake lilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Kazi yake aliyokusudiwa ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaweza kulipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Mm! Kwa nini alingojea BWANA ASEMA HIVI?

79 Yeye alitaka, "Bwana, nifanyeje? Hapa nimewaleta hawa wana, umbali huu. Hii hapa hali, Farao anakuja. Wote watakufa. Nifanye nini? Nifanye nini?" A-haa! A-haa!

Alikuwa tayari amebashiri kile watakachofanya. Aliisha kusema kile hasa, watakachofanya. Alibashiri mwisho wa taifa alimolewa. Natumaini mnaelewa. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnaona? Musa

alikuwa tayari amesema, "Hutawaona tena. Mungu atawaangamiza. Wamewadhihaki muda mrefu kutosha. Mungu atawaangamiza." Tayari aliisha bashiri yatakayowapata.

Basi, "Bwana, nifanye nini?" Mnaona tabia ya binadamu hapo? Mnaona? "Nifanye nini? Nitangojea BWANA ASEMA HIVI." Naam, bwana. "Nitaona yale Bwana asemayo, ndipo nitafanya hivyo." A-ha!

Kumbukeni, kulikuweko na farao aliyekuwa ameinuka asiyemjua Yusufu, mnajua, wakati huo, wakati uo huo. Mnaona? Mnaona? Naye Musa akasimama moja kwa moja na kutabiri mwisho wa taifa hilo.

80 Na hapa alikuwa moja kwa moja mahali ambapo jambo hilo lingetukia, ndipo anapaza sauti, "Nifanye nini, Bwana? Nifanye nini?" Mnaona? Si hao ni wanadamu? Hiyo si ni tabia ya kibinadamu tu? "Nifanye nini?" A-ha!

Alikuwa tayari, ametabiri. Mungu alikuwa ameheshimu kila kitu alichosema, naye aliitwa kwa ajili ya kazi hiyo, kwa hiyo kwa nini ilimbidi kusema, "Nifanye nini?" Kulikuwa na haja; ilikuwa ni juu yake kusema jambo hilo. Mungu alimtaka Musa kuweka kipawa hicho cha imani, ambacho alikuwa amempa, kufanya kazi. Mungu alikuwa amelithibitisha. Ilikuwa ni Kweli. Naye Mungu alimtaka Musa, alitaka watu waone ya kwamba Yeye alikuwa pamoja na Musa.

Naye, huko nyuma, alingojea, kasema, "Sasa, Bwana, mimi ni mtoto tu. Hebu Wewe uniambie sasa."

"Naam, nitaenda nikafanye *hivi*. Nina BWANA ASEMA HIVI."

"Ndugu, je! Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI?"

"Naam, naam," Ndugu Musa, "hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Naam."

"Sawa, tumelipata sasa, BWANA ASEMA HIVI." Nayo ikatendeka. Haikukosa kutimia hata wakati mmoja. Haikukosea kamwe.

Ndiyo hii tena chini ya hali ya mambo, yakazuka tena. Sasa amewafanya washike safari. Kanisa tayari limeitwa litoke, amewaingiza safirini, nao wanasonga mbele. Ndipo Musa akaanza kupaza sauti, "Bwana, ni BWANA ASEMA HIVI? Nifanye nini?" Vema.

81 Mungu alimtaka Musa kuwa na imani, apate kuitumia hiyo, karama ambayo tayari a—ameithibitisha dhahiri. Mungu alikuwa amemthibitishia Musa na watu dhahiri ya kwamba ilikuwa ni Yeye, kwa Neno na kwa mambo yaliyosemwa yakatimia. Ilitambulishwa dhahiri. Hapakuwepo haja kwake kuhofu tena kuhusu hayo. Mnaona? Hapakuwepo haja kwa kuwazia cho chote juu yake, kwa maana tayari ilikuwa wazi. Alikuwa tayari amefanya mambo haya. Aliisha kuthibitisha kwa inzi na viroboto ya kwamba alinena kisha vitu vikaumbika, ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa ndani yake.

Kwa hivyo hapa yuaenda kumuuliza Mungu la kufanya, wakati mambo yanamkabili yeye. Mnaona? Loo, jamani!

Natumaini jambo hili litatufikia, nasi tunaweza kuona mahali tulipo. Mnaona? Si inakufanya ujisikie mkubwa *hivi*? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Tukiwazia habari za Musa, tukizungumza kuhusu makosa yake, na kutazama yale yetu. Naam. Mnaona?

82 Hapa alikuwa anasimama pale, mnaona, alijua ya kwamba Maandiko yalisema kwamba hiyo ilikuwa ndiyo saa na siku kwa hayo kutendeka, naye alijua ya kwamba Mungu alikuwa amekutana naye katika Nguzo ya Moto. Nayo ilishuka moja kwa moja mbele za watu na kufanya miujiza hii. Na kila kitu alichosema, kilitimia, hata kuleta vitu katika uumbaji. Akifanya mambo ambayo Mungu pekee angeweza kufanya, akionesha ya kwamba sauti yake ilikuwa ni Sauti ya Mungu.

Na hapa hali ya mambo ikatukia kati ya watu aliokuwa akiwalea, akiwaongoza hata kwenye Nchi ya Ahadi, na huku anasimama akilia, "Nifanyeje?" Huyu ni mwanadamu, anayetaka kuninii tu ...

Kama vile Ndugu Roy Slaughter, ninaamini ameketi nje ya mlango pale, alivyoniambia wakati mmoja, kuhusu mtu fulani akinifanyia jambo fulani. Nami nikasema, "Vema, nilifanya *hili*, na sasa ni *lile*."

Naye akasema, "Ndugu Branham, waache waagemee mabegani mwako, na kesho utawabeba." Na hivyo ndivyo binadamu alivyo. Wanaegemea mebegani mwako leo, na kesho unawabeba.

Hivyo ndivyo ilivyo, hivyo ndivyo Musa alivyokuwa akifanya. Ilimbidi Mungu kumchukua baada ya kumchagua na kumthibitisha kufanya hivyo. Nao watu walipaswa kusema, "Musa, sema neno. Nilikuona ukifanya jambo hilo *pale*. Mungu alikupa heshima pale, nawe ni yeye yule leo." Amina. Mnaona? "Fanya hivyo!" Amina. Alipaswa kujua jambo hilo, bali hakujua. Vema. Kama tu ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa. Tunaona, kwamba. Kwa hivyo yeye akasema...

83 Hapana shaka Mungu alikuwa amechoka nayo. Hapana shaka Mungu alichoshwa nayo. Yeye alisema, "Mbona unanililia Mimi? Je, Mimi sijathibitisha utambulisho Wangu tayari? Si niliwaambia ya kwamba

nilikutuma kwa ajili ya kazi hiyo? Sikukuambia uende ukafanye hili? Sikuahidi ya kwamba ningetenda haya; ya kwamba ningekuwa pamoja kinywa chako, nami ningenena kupitia kwako nami ningefanya hivi, nawe uonyeshe ishara na maajabu? Si niliahidi kufanya hivyo? Si nimefanya hivyo kabisa, na mimi sijaangamiza kabisa kila adui aliyekuzingira? Na ndiwe huyu hapa umesimama hapa sasa kwenye Bahari ya Samu, ukitenda niliyokwambia kutenda, na ungali unapiga makelele na kunililia Mimi. Je, unaniamini Mimi? Je, huwezi kuona ya kwamba nilikutuma kufanya hivi? Loo, kama huyo si ubinadamu! Jamani! Kwa hivyo hapana budi ilimchosa kabisa.

84 Naye akasema, "Unajua unaihitaji. Unajua kama utawapeleka hawa wana kule katika Nchi ya Ahadi. Hiyo ni kweli kabisa. Umesongwa hapa pembeni. Hamna cho chote kingine unachoweza kufanya. Kwa hiyo kuna haja. Kwa nini unanililia Mimi? Mnaniangalia Mimi kwa nini? Unaniitia nini? Je, sijathibitishia watu? Sijakuthibitishia? Sijaiita? Si ni kulingana na Maandiko? Sikuahidi kuwapeleka watu hawa katika ile nchi? Sikukuita na kukuambia ya kwamba ningefanya hivyo? Sikukuita na kukwambia nimekutuma kufanya hivyo, na haikuwa wewe, ilikuwa Mimi? Nami nitashuka na nitakuwa pamoja na kinywa chako, na cho chote ulichosema, nilikithibitisha na kukishuhudia. Si nimefanya hivyo?"

"Basi wakati jambo lo lote ndogo linapozuka, mbona unatenda kama mtoto? Unapaswa kuwa mwanamume. Nena na watu," amina, "kisha songeni mbele!" Amina. Haya basi. "Usilie. Nena!" Amina. Loo, napenda jambo hilo. "Mbona unanililia? Nena tu na watu kisha songeni mbele kwa shabaha yenu." Cho chote kile, kama ni magonjwa, cho chote kile, kama ni kufufua wafu, ama cho chote kile, nena! Nilithibitisha hayo. Nena na watu."

85 Ni somo lililoje! Ni somo lililoje, loo, jamani, katika hatua hii ya safari ambapo tunasimama. Angalia mahali tulipo sasa, naam, bwana, kwenye ule Mvuto wa Tatu. Angalia, tuko papa hapa mlangoni, juu ya Kuja kwa Bwana.

Alikuwa ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi hiyo, na angali akingojea BWANA ASEMA HIVI. Hapana shaka Mungu alichoshwa na hayo. Yeye alisema, "Usilie tena. Nena! Nilikutuma."

Ee Mungu, jinsi Kanisa hili linavyopaswa kuwa asubuhi ya leo! Pamoja na thibitisho kamilifu la Mungu, pamoja na Nguzo ya Moto na ishara na maajabu, kila kitu kama tu ilivyokuwa katika siku za Sodoma. Alisema zitajirudia.

Huu hapa ulimwengu katika hali yake. Hilo hapo taifa katika hali yake. Hao hapo wanawake walio katika hali hiyo. Huyu hapo mtu aliye katika hali hiyo. Hilo hapo kanisa katika hali hiyo. Kuna kila kitu. Vitu asili, zile ishara, visahani virukavyo angani na kila kitu angani, na kila namna ya vitu vya ajabu, na bahari ikiunguruma, mawimbi ya baharini, watu wakivunjika mioyo kwa hofu, uoga, mashaka ya nyakati hizi, na dhiki ya mataifa, kanisa likianguka.

86 Na yule mwasi akiinuka, ambaye hujiinua juu ya yote; yaitwayo Mungu, yeye aketiye katika hekalu la Mungu, akijionesha nafsi yake, loo, jamani, naye amezuru taifa hili. Na kanisa limeunda shirika, nao wote wamekusanyika pamoja kama malaya wa yule kahaba, na kila kitu kimeingilia ukahaba.

Ukahaba, ni nini? Kuwaambia wanawake wanaweza kukata nywele zao, kuwaambia wanawake wanaweza kuvalia kaptula, kuwaambia wanaume wanaweza kufanya *hivi* na wafanye *vile*, na mhubiri akisema, fanya *hivi*, na injili ya kijamii na kadhalika. Hivi hamwoni, huko ni kufanya uzinzi na Neno la kweli la Mungu!

Naye Mungu ametutumia Neno Lake la kweli lisilo la kidhehebu, hakuna masharti yaliyofungwa Kwake, na kutupa ile Nguzo ya Moto, Roho Mtakatifu ambaye amekuwa pamoja nasi sasa kwa miaka thelathini, Na kila kitu alichobashiri na kusema, kilitendeka vile hasa alivyosema kingetendeka.

87 Nena na watu, hebuni tusonge mbele." Amina. Tuna shabaha fulani, hiyo ni Utukufu. Hebu na tuuendee. Tunaelekea kwenye Nchi ya ahadi. "Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." "Nena na watu. Je! Sijalithibitisha. Si hata nimepigwa picha miongoni mwenu, na kila kitu kinginecho, na kufanya kila kitu ambacho kingefanywa kuwathibitishia, ya kwamba niko pamoja nanyi? Je! Magazeti haya, majuma machache tu yaliyopita, hayajabeba makala haya, wakati uliposema hapa mimbarani ni kitu gani kingetukia hapa, na miezi mitatu kabla, na hapo yakaanza kutendeka na kuthibitisha? Hata sayansi inajua habari zake. Na kila kitu ambacho nimefanya, nawe ungali unangojea. Nena na watu na msonge mbele hata kwenye shabaha yenu." Amina.

Hivi Nathani hakumwambia Daudi? Nathani, yule nabii, wakati mmoja, alipomwona Daudi yule mfalme mpakwa mafuta, alisema, "Haya, fanya yote yaliyomo moyoni mwako, kwa maana Mungu yu pamoja nawe." Alimwambia Daudi, "Fanya yote yaliyo moyoni mwako. Mungu yu pamoja nawe."

88 Yoshua alitiwa mafuta kuchukua nchi kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya watu wake. Siku ilikuwa fupi. Alihitaji wakati zaidi kwa ajili ya ile kazi aliyokuwa na upako wake na kuagizwa kuitenda. Yoshua, mtu, alikuwa ametiwa mafuta. Mungu alimwambia, "Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, nitakuwa pamoja nawe." Amina. "Nchi hiyo, nitawapa. Nami nawatakeni mwende kule na kuwasafisha Waamaleki, na—na

Wahi- ... Wote—hao wengine wote, Wafilisti na—na Waperizi, na wengine wote mbalimbali, wafagilie mbali. Niko pamoja nanyi. Nita- ... Hakuna mtu atakayesimama mbele yako, siku zote za maisha yako. Hakuna mtu anayeweza kukusumbua. Ingia mle.”

Naye Yoshua akachomoa upanga wake akasema, “Nifuateni!”

Naye akafika kule, naye hapa alikuwa akipigana. Na ilikuwa ni kitu gani? Akawashinda adui. Walikuwa vikundi vidogo hapa na vikundi vidogo *pale*. Usiku ulipofika, wote wangekusanyika na kufanya kikosi kizima, na kuja kama jeshi kubwa kupigana naye. Na jua lilikuwa likitua. Alihitaji nuru zaidi. Jua lilikuwa likitua. Yeye hakupiga magoti na kusema, “Bwana Mungu, nifanye nini? Nifanye nini?” Alinena! Alikuwa na haja. Akasema, “Jua, simama kimya!” Naye hakulia hata kidogo. Yeye aliamuru, “Jua, simama kimya! Nina haja ya jambo hili. Mimi ni mtumishi wa Bwana, nimetiwa mafuta kwa ajili ya kazi hii, nami nina haja. Simama kimya, wala usiangaze ... Na wewe mwezi, simama mahali ulipo,” hata alipomaliza vile vita na kuangamiza kitu hicho chote. Na jua likamtii.

89 Hakuna kulia. Yeye alinena na jua, akasema, “Wewe simama kimya. Jua, kaa hapo! Na, ewe mwezi, kaa mahali ulipo.” Yeye hakupaza sauti, “Bwana, sasa nifanye nini? Nipe nuru ya jua zaidi.” Alikuwa na haja ya nuru ya jua, kwa hiyo akaamuru, na jua likamtii. Loo, jamani! Yeye aliliamuru jua lisimame kimya.

Samsoni, aliyetiwa mafuta, aliinuka, amechaguliwa na Mungu, akapewa karama ya nguvu na kuagizwa kuangamiza taifa la Wafilisti. Aliagizwa, akazaliwa humu duniani, akatiwa mafuta na Mungu kuwaangamiza Wafilisti. Na siku moja wakamshika nje kondeni, bila upanga wake, bila mkuki. Nao elfu moja ya hao Wafilisti wenye silaha walimkimbilia kwa wakati mmoja. Je, yeye alianguka chini na kusema, “Ee Bwana, nangojea ono? Ee Bwana, nifanye nini? Nielekeze sasa la kufanya?” Alijua alikuwa na haja. Hakupata kitu ila taya la kale la nyumbu, naye akawapiga Wafilisti elfu moja. Amina!

Yeye hakumlilia Mungu kamwe. Alitumia kipawa chake kilichotiwa mafuta. Alijua ya kwamba alitumwa kwa ajili ya kazi hiyo. Alijua alizaliwa kwa ajili ya jambo hilo. Alijua alikuwa ametiwa mafuta kwa kipawa, naye akawapiga Wafilisti elfu moja. Yeye hakumlilia Mungu. Mungu alimchagua na kuthibitisha kwamba alikuwa hivyo, kwa mambo mengine aliyokuwa amefanya. Naye alikuwa mtumishi wa Mungu aliyethibitishwa, aliyetiwa mafuta, kuwaangamiza Wafilisti, naye akafanya hivyo. Haidhuru hali ilikuwaje, alifanya hivyo. Kamwe hakuuliza kitu. Hiyo ilikuwa ndiyo kazi yake. Kwamba, Mungu alikuwa akitenda kazi kupitia kwake; alichukua mfupa ule wa nyumbu na kuanza kuwapiga Wafilisti. Jinsi ninii ...

90 Mbona, pigo kwa kitu hicho juu ya hizo fuvu za kichwa upana wa ichi moja na nusu ya shaba zingaliuvunjavunja mfupa huo katika vipande milioni moja. Na akawapiga elfu moja yao, na kuwaua na bado akasimama nacho mkononi mwake.

Hakuuliza maswali yo yote. Hakulia. Alinena. Akawashinda. Loo, jamani! “Twa Wafilisti, “naweza kuwatwaa Wafilisti, Bwana? Ni-ninajua ulinituma kufanya hivyo Bwana. Naam, Bwana, ninajua Wewe ulinituma kuliangamiza taifa hili la Wafilisti. Sasa hapa, elfu yao wamenizinguka, nami sina kitu. Nini, nitafanya nini sasa, Bwana?” Loo, jamani! Hakuna kitu kitakachomsumbua. Yeye ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi hiyo. Hakuna kitu kinachoweza kukudhuru. La, hakuna hata jambo moja. Haleluya! Alichukua alichokuwa nacho na kuwapiga. Hiyo ni kweli.

91 Adui alipomzingira na kusema, “Sasa tunaye ndani ya kuta, tumempata sasa. Tumemshikia upande wa ndani huku akiwa na mwanamke. Sasa tumefunga mlango, kila mahali, naye hawezi kutoka. Tumempata.”

Samson hakulia, “Ee Mungu, wamenizingira kila mahali kwa hili dhehebu.” A-ha! “A-ha, nitafanya nini? Nimejiunga nao. Nitafanya nini?” Kamwe hakufanya hivyo.

Aliondoka tu, akang'oa hilo lango, akaliweka begani mwake na kuondoka nalo. Amina! Alikuwa ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi hiyo. Yeye aliitwa na Mungu. Hawakumfungia ndani. La, hakika! Aliondoka na hayo malango. Yeye hakuomba juu ya jambo hilo. Yeye hakumwuliza Mungu kama afanye hivyo au la. Ilikuwa moja kwa moja kwenye wajibu wake. Amina, amina, amina! Moja kwa moja kazini mwake. “Mbona kunililia Mimi? Nena, na uendele!” Amina! “Usilie. Nena!” Aliisha koma kulalamika na kulialia sasa. Alipaswa kuwa na umri wa kutosha kunena. Hiyo ni kweli. Alijua ya kwamba kipawa chake kilichotiwa mafuta ya nguvu ingeamamiza Mfilisti ye yote aliyesimama mbele yake. Amina.

92 Lakini hatujui jambo hilo, mnaona. Tungali watoto wachanga, na tukiwa na chupa mdomoni mwetu.

Alijua jambo hilo, alijua ya kwamba Mungu alimwinua kwa kusudi hilo, wala hakukuwa na kitu kitakachosimama mbele zake, siku zote za maisha yake. Hakuna kitu kingeweza kumwangamiza. Yeye aliinuliwa kwa kusudi hilo, kama vile Musa alivyoinuliwa. Hakuna kitu kitakachomzuia. Hakuna Waamaleki wala kitu kingine chochote kinachoweza kumzuia. Yeye yuko njiani akielekea kwenye nchi ya ahadi. Samsoni alijua alikuwa njiani.

Yoshua alijua alikuwa akiitaka hiyo nchi. Yeye alikuwa amethibitishwa. Neno la Mungu liliahidi jambo

hilo, na Roho Mtakatifu alikuwa pale akilithibitisha.

93 Alikuwa njiani, kwa hiyo hakukuwa na kitu kitakachomzuia. La, bwana. Moja kwa moja kwenye wajibu wake, pamoja na Mungu, hakuna kitu kitakachomzuia. Kwa hiyo akachukua tu malango na kuyaweka begani mwake, yalikuwa na uzito wa kama tani nne ama tano, kisha akapanda juu ya kilima na akayakalia. Hakuna kitu kitakachomzuia. Alikuwa na kipawa kilichotiwa mafuta kutoka kwa Mungu. Haikumlazimu kulia, "Bwana, nifanyeje sasa?" Yeye alikuwa tayari ametiwa mafuta kufanya jambo hilo. Hiyo ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI, "Waondoe!" Haleluya! "Waangamize! Nimekuinua kwa kusudi hilo." Amina.

"Nifanye nini, Bwana? A-ha, nitafanya nini hapa kwenye Bahari ya Shamu?"

Je, sikukuambia ya kwamba nilikupa mlima kama ishara papa hapa? Utarudi kwa huo mlima, utawapeleka hawa wana katika hiyo Nchi. Sikukuita kwa kusudi hilo? Kwa nini unahofu juu ya jambo jingine lo lote kukuzuia? Nena, na uanze kusonga mbele!" Amina na amina! "Naam, nilikuita kwa kusudi hili."

94 Daudi, alijua alikuwa ametiwa mafuta, na alikuwa amethibitishwa kuwa ni mtu mzuri. Yeye alijua ya kwamba alikuwa na shabaha mzuri. Daudi alitiwa mafuta. Yeye anajua jambo hilo. Na wakati aliposimama mbele ya Goliathi, hakupaza sauti, "Ee Mungu, nifanyeje sasa? Ngojeni, lazima ni—ni ... Ninajua yale uliyofanya katika nyakati zilizopita. Wewe, uliniacha niue dubu, na Wewe uliniacha niue simba. Lakini vipi kuhusu huyu Goliathi huko nje?" A-ha! Kamwe hakufanya hivyo. Yeye alinena tu. Yeye alisema nini? "Utakuwa kama walivyokuwa, machoni pako." Alinena na akasonga mbele.

Kamwe hakuomba maombi. Hakusali hata kidogo. Alijua alikuwa ametiwa mafuta. Amina. Yeye alikuwa amepakwa mafuta na hilo pigo la kombeo lilithibitisha jambo lililosahihi. Alikuwa na imani katika upako wake. Aliamini ya kwamba Mungu angeongoza hilo jiwe moja kwa moja hata katikati ya hiyo kofia ya chuma ambapo ndipo tu mahali pangeweza kupigwa. Alikuwa amesimama pale.

95 Alijua alikuwa na shabaha nzuri. Amina. Alijua Mungu alimfanya hivyo. Amina. Alijua aliisha muua simba, alijua aliisha muua dubu, bali hiyo ilikuwa kwa mali ya baba yake wa duniani. Hapa kuna mali ya Baba yake wa Mbinguni! Amina. Hakushuka chini, "Lazima ... Nifanye nini sasa, Bwana?" Yeye alinena na kusema, "Mtakuwa kama simba na dubu, nami hapa ninakuja." Amina! Utukufu kwa Mungu! Naam, bwana. Alinena na akasonga mbele kukutana na huyu Goliathi. Loo, jamani!

Bila kujali ukubwa wake! Alikuwa jamaa mdogo, aliyekana mwekundu, mnajua. Yeye hakuwa mkubwa sana. Hakuwa mwenye sura nzuri sana ukimtazama, kijitu cha mtu. Biblia ilisema alikuwa mwekundu. Sasa, bila kujali ukubwa wake na kile kinachoitwa uwezo wake wa kufanya hivyo.

Mwajua, yule—yule askofu alimwambia, kasema, "Sasa angalia hapa, mwanangu, mtu huyo ni mwanatheolojia. Mnaona, yeye ni mpiganaji. Alizaliwa mpiganaji na yeye ni ... Yeye amekuwa mpiganaji, tangu ujana wake; wala hufanani naye." Na ndugu zake wakasema, "Lo, mtukutu wee! Unakuja humu na kufanya jambo kama hilo, rudi nyumbani."

Hilo halikumsumbua. Kwa nini? Alijua alikuwa ametiwa mafuta. "Mungu aliyenikomboa kutoka kwa yule simba, Mungu aliyenikomboa kutoka kwenye makucha ya dubu huyo, atafanya zaidi ya hayo, ataniokoa kutoka kwa yule Mfilisti. Mimi hapa ninakuja. Ninakutana nawe katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli." Amina. Hakuomba hata kupata ushindi; alikuwa tayari ameomba kutosha. Mungu alimwomba kutosha kabla kuweka misingi ya ulimwengu. Alikuwa ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi hiyo. Ilimbidi kuzungumza na kusonga mbele. Hilo tu ndilo lililokuwako juu ya jambo hilo, kunena tu na kusonga mbele. Loo, hivyo tu ndivyo ilivyokuwa. Loo! Yeye hakuninii ...

96 Kuhusu ndugu zake wa kidini, hao wenye kudhihaki wakisimama pale, pia, mnajua. Loo, naam. Walikuwa wamesimama pale wakisema, wakidhihaki na kufanya mzaha, na kusema ... Ndugu zake, mnajua, na kusema, "Ah, ah, ah, huwezi. Wewe, mtukutu tu wewe." Hilo halikumtikiza hata kidogo. "Unataka kuwa tofauti na mtu mwingine. Unataka kujionyesha tu." Kama hiyo ilikuwa kujionyesha, ingekuwa hivyo. Lakini wao waliangalia tu upande wa kiakili.

Daudi alijua mafuta ya upako yalikuwa juu yake. Amina. Haikuleta tofauti yoyote kwake. Yeye alisema, "Huyo Mfilisti atakuwa kama dubu na simba, kwa hiyo mimi hapa ninakuja." Yeye alibashiri jambo hilo kabla halijatukia. Alifanya nini? Alimwua dubu. Alimwua simba. Alimwangusha simba chini kwa ... Na nini? Akiwa na—na kombeo, na akachukua kisu, halafu dubu. Simba, alimwua simba kwa kisu. Hivyo ndivyo alivyomfanyia Goliathi. Alimwangusha kwa jiwe, kisha akauchomoa upanga wake, akakikata kichwa chake papo hapo mbele yao. Alitabiri nini kabla halijatukia? "Nawe utakuwa kama wao." Kwa nini? Alinena neno ya kwamba itakuwa hivyo, ndipo akasonga mbele kulifanya litimie. Amina. Loo, ndugu! Yeye alinena, na kuchukua hali siku hiyo.

97 Kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo mwanadamu anapaswa kunena, ni sasa. Kufunga, dakika chache tu zifuatazo kama unaweza tu kuvumilia kwa dakika chache zaidi. Nina mambo mengine zaidi

yaliyoandikwa hapa, Maandiko fulani ninayotaka kuyaandika.

Petro hakulia kamwe, alipompata mtu aliyekuwa na imani ya kutosha kuponywa, amelala kwenye lango liitwalo Mzuri. Hakupiga magoti na kuwa na maombi ya usiku kucha, na, ama maombi ya mchana kutwa, ama ombi refu sana na kusema, "Bwana, nakuomba, Wewe sasa, ya kwamba utamsaidia maskini mtu huyu kiwete. Ninaona ya kwamba ana imani. Ninajua yeye ni mwamini. Nami nimemwuliza, naye—yeye ... Ni—ni—ni ... Yeye alisema alikuwa na imani, angeamini yale niliyomwambia. Nami nimemwambia kuhusu ninii ... kuhusu yale uliyofanya, nami na—nafikiri tu sasa, Bwana, ya kwamba—ya kwamba ... Waweza kunipa BWANA ASEMA HIVI kwa ajili yake?"

Hasha, alijua ya kwamba alikuwa mtume mtiwa mafuta. Alijua ya kwamba Yesu Kristo alimwagiza. "Waponye wagonjwa, ufufue wafu, safisha wenye ukoma, toa pepo. Kama mliyopata bure, toeni bure." Akasema, "Petro, nenda kafanye hivyo!" Haikumlazimu kuomba. Yeye aliagizwa.

98 Yeye alisema nini? Yeye alisema, "Katika Jina la Yesu Kristo!" Yeye alitaja Jina la Yesu Kristo, naye huyo mtu akaketi tu pale. Naye akamshika mkono, na kusema, "Simama kwa miguu yako!" Naye akamshikilia pale mpaka mifupa yake ya kifundo cha mguu ikapata nguvu, naye akaanza kutembea. Kwa nini? Hakuwa na mkutano wa maombi usiku kucha. Yeye hakumlilia Mungu kamwe. Yeye alijua dhahiri, kutoka kinywani mwa Yesu Kristo, alikuwa ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi hii. Naam. Yeye alinena na kumwinua, kwa kuwa alijua alikuwa mtume aliyetiwa mafuta kwa kusudi hilo.

Watu waliolala katika kivuli chake kamwe hawakusema, "Loo, njoo, mtume Petro, ukatulilie, na utuombe maombi ya imani, kwa Mungu." La, la, kamwe hawakusema jambo hilo. Walijua alikuwa ametiwa mafuta na mtume wa Mungu aliyethibitishwa. Kwa hiyo walisema, "Hebu na tukae katika kivuli chake. Haikubidi kusema neno. Tunajua jambo hilo. Tunaamini." Uhai uliokuwa ndani yao! Yule mtume asingeweza kuwafikia wote. Nao, wao wenyewe, wao ni sehemu yake.

99 Musa alisema, "Si mimi tu ninayeenda. Sote tunaenda." Sisi sote tuna jambo la kufanya. Sote hatuna budi kutiwa mafuta.

Nao walimwona huyo mtume akisimama pale, na kumwona akimponya huyo mgonjwa na kufanya mambo aliyofanya. Wanajua asingeweza kuwafikia. Kasema, hawakusema kamwe, "Petro, njoo na—na uombe, na subiri sasa mpaka utakapopata BWANA ASEMA HIVI, na uje uniambie. Angalia yale asemayo Bwana." Walisema, "Laiti tungaliweza kukaa katika kivuli chake, kwa sababu Mungu yeye yule aliyekuwa ndani ya Yesu Kristo yumo ndani yake, nasi tunaona jambo lile lile likitenda. Kwa hivyo akagusa upindo wa vasi la Yesu na kujilaza kivulini mwake, na Yesu alikuwa katika mtu huyu. Kama kivuli hicho kikituangukia, tutaponywa.

Na Biblia ilisema kila mmoja wao aliponywa. Hakuna mkutano wa maombi ya usiku kucha, ukisema, "Bwana, kama nikienda kulala katika vivuli vya mtume huyu?" La, walijua jambo hilo. Nuru ilikuwa imewagusa. Mioyo yao ilikuwa imejaa. Imani yao ilifunguliwa. Amina. Waliamini. Walikuwa wameiona. Leso za Paulo, vile vile.

Sasa, katika kufunga.

100 Yesu kamwe hakulia wakati walipomleta yule kijana mwenye kichaa Kwake, aliyekuwa na kifafa, akianguka motoni. Yeye kamwe hakusema, "Baba, Mimi ni Mwanao, na sasa Wewe ulinituma hapa kufanya jambo *fulani*, na kadhalika. Naweza kumponya mvulana huyu?" Yeye hakusema kamwe. Akasema, "Toka ndani yake, Shetani!" Alinena, naye mvulana huyu akapona.

Wakati alipokutana na yule Legioni mwenye mapepo elfu mbili ndani yake, haikuwa Yesu akilia. Ilikuwa ni pepo wakilia, "Kama utatutoa," loo, jamani, "turuhusu tuingie kwenye lile kundi la nguruwe."

Yesu kamwe hakusema, "Sasa, Baba, je! Ninaweza kufanya jambo hili?" Yeye alisema, "Tokeni kwake," na pepo wakaondoka. Hakika, Yeye alijua alikuwa Masihi.

101 Kwenye kaburi la Lazaro, alikuwa amekufa siku nne. Wao walisema, "Kama ungalikuwa hapa, Bwana, asingalikufa."

Yeye alisema, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima." Amina! Si wapi, lini, ama vipi. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi." Amina. Yeye alijua alikuwa ni Nani. Yeye alijua kile alichokuwa. Alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Imanueli. Yeye alijua alikuwa ufufuo. Yeye alijua alikuwa Uzima. Yeye alijua ya kwamba ndani Yake mlakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Yeye aliwaona hao watu wadogo pale, na alikuwa ameona yale Mungu aliyomwambia atende wakati huo, na huyo hapo. Alishuka akaenda kule.

Kamwe hakusema, "Sasa, ngoja, nitapiga magoti hapa. Ninyi nyote pigeni magoti na kuomba." Akasema, "Unaamini ya kwamba ninaweza kufanya jambo hili?" Amina. Aliomba.

Haikuwa Yeye; ilikuwa ni wao. "Naam, Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu aliyekuwa aje ulimwenguni." Loo, jamani! Hapo Yeye ametambulishwa. Jambo fulani halina budi kutukia.

“Lazaro, njoo huku!” Yeye alinena, na mtu aliyekufa akatokea. Si, “naweza?” Yeye alinena tu. Wakati imani ilipotimizwa, jambo hilo lilitukia.

102 Yeye hunena, alinena, na vipofu wakaona, viwete wakatembea, viziwi wakasikia, pepo wakapiga makelele na kutoka, wafu wakafufuliwa, kila kitu. Kwa nini? Yeye hakuomba hata akapata ushindi. Yeye alikuwa Masihi mtiwa mafuta. Yeye alikuwa ndiye huyo Masihi. Alijua alikuwa hivyo. Yeye alijua mahali Pake. Yeye alijua kile alichotumwa kufanya. Yeye alijua ya kwamba Baba alikuwa amemtambulisha kuwa Masihi, kwa mwamini. Na wakati alipokutana na huyo mwamini kwa imani, Yeye alinena tu Neno. Mashetani walitawanyika. Naam, Bwana. “Nena! Usilie. Nena!” Amina.

Naye alijua haki Zake alizopewa na Mungu, bali hatujui. Yeye alijua kile alichokuwa. Sisi hatujui.

Musa alikuwa amesahau. Samsoni alielewa. Wengine walielewa. Yoshua alielewa. Musa alisahau. Ilimbidi Mungu kumkumbusha. Alisema, “Mbona unanililia Mimi? Nalikutuma kufanya hiyo kazi. Nena, na uende kwenye lengo lako. Niliwaambia mngekuja kwenye mlima huu. Ukawachukue hao wana uwaongoze. Nena tu. Sijali kilicho njiani mwako, kiondoe njiani. Ninawapa mamlaka ya kufanya jambo hilo. Nilinena ... Umenena nzi na viroboto, na uumbaji, na mambo kama hayo. Sasa unanipigia kelele kwa nini? Mbona unakuja Kwangu, ukipiga makelele juu ya mambo haya? Nena tu uone ikitendeka, hivyo tu.” Loo, jamani! Loo, jinsi nependavyo hilo.

103 Hapa, Yesu, kila kitu alichosema, Yeye alinena tu Neno, na ikawa hivyo. Mungu kikamilifu alikuwa amemthibitisha kuwa Mwanawe. “Huyu ni Mwanangu mpendwa Ambaye nimependezwa Naye. Msikieni Yeye.”

Mtazame. Ninapenda jambo hili. Jinsi alivyosimama kwa ujasiri, na fahari mbele ya wapinzani wakosoaji Wake. Amina. Yeye alisema, “Liharibuni hekalu hili, nami nitamwomba Baba na kuona kile atakachofanya juu yake?” “Liharibuni hekalu hili, nami nitalijenga tena, katika siku tatu.” Si kwamba, “Natumaini; Nitajaribu kufanya hivyo.” “Nitalifanya hivyo!” Kwa nini? Maandiko yalisema hivyo.

Andiko lile lile lililosema Yeye angeufufua mwili Wake, linatupa mamlaka, zNguvu. Amina! “Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya; kama wakishika nyoka, ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

“Kwa nini mnililie? Nena, na usonge mbele.” Loo, kwa ujasiri mimi ...

“Liharibuni hekalu hili, nitalijenga tena.” Loo!

104 Na kumbukeni sasa, (tunafunga), ilikuwa ni Yeye yule yule. Ni Yeye aliyesema, katika Yohana 14:12, ninii ... “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Ni Yeye aliyesema hivyo.

Ilikuwa ni Yesu, katika Marko 11:24, aliyesema, “Ukiambia mlima huu,” si kama ukiomba mlima huu. “Ukiambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali amini ya kwamba uliyosema yatatimia, unaweza kupata yale uliyosema.” Sasa, kama ukisema tu kwa kubahatisha, haitatendeka. Lakini kama mna kitu ndani yako, ya kwamba—umetiwa mafuta kwa kazi hiyo, na utajua kwamba ni mapenzi ya Mungu kufanya hivyo, na utasema hivyo, haina budi kutendeka. “Kama ninii ...”

Ni Yeye aliyesema jambo hili. “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtapewa.” Loo, jamani! Loo, jamani! Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.]

105 Samahani hili, bali linakuja tu ndani yangu. Sina budi kulisema. Ni Yeye aliyesema, siku hiyo kule juu, ndani ya mwitu huo, “Hamna wanyama wa kuwinda.” Naye akaumba kindi watatu wakisimama pale mbele yetu. Ni kitu gani? Nikinena tu neno, kusema, “Watakuwa *pale*, na *pale*, na *pale*,” na hao hapo. Ni Yeye aliyefanya jambo hilo.

Charlie, Rodney, ilikuwa Yeye kule chini Kentucky; na Nellie, Margie, na wengine wenu. Ilikuwa ni Yeye, Mungu yeye yule aliyekuwa nyuma kule na kunena na Musa, alisema, “Mbona mnanililia Mimi? Nena neno!” Yeye ndiye aliyewaumba. Ni Yeye. Ni Yeye. Loo, jamani!

Ilikuwa ni Yeye aliyenipa lile ono yapata mwaka mmoja uliopita, lililosema tungeenda kule, na hii Mihuri Saba, na jinsi kungekuweko na—na—na—na ngurumo kubwa itakayonguruma, na itakuwa mfano wa piramidi. Na hapo gazeti la *Look* mag- ... Gazeti la *Life* limeandika, likining'inia ukutani mle ndani. Ni Yeye aliyesema hivyo.

106 Ilikuwa ni Yeye, usiku huo wakati nilipokuwa nikishuka kwenda barabarani na kumwona yule nyoka mwenye sumu sana aitwaye mamba akiwa karibu kumgonga ndugu yangu. Yeye akasema, “Umepewa ... nguvu za kumfunga ama wengine wote.” Ni Yeye aliyesema jambo hilo.

Ilikuwa ni Yeye aliyemwambia huyo maskini mke wangu anayeketi kule nyuma—ilikuwa Ndiye ile

asubuhi aliyeniamsha chumbani na nikiketi pembeni akisema, "Usiogope kufanya cho chote ama kwenda po pote ama kusema cho chote, kwa maana uwepo usioshindwa wa Yesu Kristo uko pamoja nawe po pote uendako."

Ilikuwa ni Yeye kule ng'ambo ya Sabino Canyon, yapata miezi mitatu iliyopita, nilipokuwa nikiimba, nikishangaa ni kitu gani kitakachotukia. Nilikuwa nimesimama pale, na upanga ulianguka mkononi mwangu, na kusema, "Huu ni ule Upanga wa Mfalme." Ilikuwa ni Yeye.

Ni Yeye aliyeniambia, "Kama vile nilivyokuwa pamoja na Musa, vivyo hivyo nitakutuma."

107 Ni Yeye aliyeniambia, miaka thelathini iliyopita, kule chini mtoni, kama mvulana mdogo. Nimesimama mle kama mhubiri kijana, mtoni miaka thelathini iliyopita, nimesimama mle wakati ile Nuru, na Nguzo ya Moto ile ile, iliposhuka kutoka mbinguni na kusimama kule, na kasema, "Kama nilivyomtuma Yohana Mbatizaji kukutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangulia kule kuja kwa pili," ulimwenguni kote. Ingewezekanaje, wakati mchungaji wangu mwenyewe aliicheka na kuifanyia mzaha? Lakini ilitukia vivyo hivyo hasa. Yeye ndiye aliyesema jambo hilo. Naam, bwana!

Loo, jinsi ilikuwa ni Yeye aliyesema katika unabii, "Itatimia." Ndiye aliyesema, "Kama mmoja miongoni mwenu anatoa unabii, ama kuona ono, na kulinena, nalo linatimia, basi kumbukeni huyo siye, ni Mimi. Niko pamoja naye." Loo, jamani! Ningeendeleaje, na kusema ni Yeye, ni Yeye, ni Yeye!

108 Ni Yeye aliyeshuka, nilipowaambia ya kwamba Nguzo ya Moto ilikuwa chini kule mtoni, nao hawakuweza kuamini. Ilikuwa ni Yeye kule chini miongoni mwao, wakati yule mhubiri Mbaptisti, mbele ya watu elfu thelathini usiku huo, katika ukumbi wa Sam Houston, wakati yule Malaika wa Bwana alipopigwa picha Yake, amesimama pale. Ilikuwa ni Yeye, yeye yule jana, leo, na hata milele.

Yeye Ndiye aliyetabiri mahali ambapo mambo haya yatakuwa. Ni Yeye aliyesema jambo hili. Ni Yeye aliyefanya mambo haya. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye amefanya kila kitu kama tu alivyosema angefanya. Amina.

Kwa nini nisubiri? Mungu amelithibitisha Neno. Ni Kweli. Hebu na tusafiri. Hebu na tutembe. Tushike njia ya Bwana, tukiweka kando mashaka yote, dhambi zote. Tuisafishe nyumba; tuisugue sana.

Kama vile ono la Junior Jackson lilivyosema, hakukuwa na kitu kilichosalia ila taa; ama ndoto yake, kama ameketi hapa. Hamna kilichosalia ila taa, nazo zilizungushiwa milia ya dhahabu, katika doto aliyonisimulia mimi majuzi usiku. Loo, jamani!

109 Ndugu Collins, usijali kuhusu samaki huyo. Alikuwa ni mweupe. Hukujua jinsi ya kulishughulikia.

Weka kando cho chote kilicho kinyume chake. Kumbukeni, hii ni Kweli, haidhuru inaonekana ya ushupavu jinsi gani, na cho chote kile, wakati mwingine. Endelea moja kwa moja na Hilo. Ni Roho Mtakatifu. Mungu yule yule aliyemfufua Yesu Kristo katika wafu, Yeye yule ambaye anaweza kunena mambo yakawa, Yeye yule aliyeishi katika siku za Musa, ni yeye yule leo.

Mwito Wake katika hizi siku za mwisho, Yeye tayari amethibitisha. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Ametenda... Kuna Sodoma kule chini. Kuna Billy Graham na Oral Roberts huko nje. Nalo Kanisa linasonga mbele, kwa ishara zile zile ambazo Yeye aliahidi, sehemu zote mbili, na hao hapo. Ni Yeye aliyesema jambo hilo.

Ee Bwana, nipe ujasiri, ndilo ombi langu. Nisaidie, Ee Bwana Mungu.

Sina budi kuachia hapa. Tumachelewa.

110 "Mbona unalililia Mimi? Kwa nini mnanililia Mimi, wakati nimethibitisha kuwa pamoja nanyi? Je! Sijawaponya wagonjwa wenu," Yeye angesema? "Hivi sijakwambia mambo yaliyotukia hasa? Mchungaji wako hawezi kufanya hivyo. Mimi! Hawezi; yeye ni mwanadamu. Ni Mimi, Bwana," ndivyo angesema. "Mimi Ndiye niliyefanya jambo hili. Mimi Ndiye ninayemwambia mambo haya ya kusema. Si yeye. Ni Sauti Yangu. Mimi ndimi ninayewafufua wafu wenu watakapoanguka. Mimi Ndiye ninayewaponya wagonjwa. Mimi Ndiye ninayetabiri mambo haya. Mimi Ndiye ninayeokoa. Mimi Ndiye ninayetoa ahadi."

Mungu, nipe ujasiri kuuchukua huo Upanga wa Neno ambao aliweka mkononi mwangu yapata miaka thelathini na mitatu iliyopita, na kuushikilia na kusonga mbele kuelekea kwenye Mvuto wa Tatu, ndilo ombi langu.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

111 Baba wa Mbinguni, wakati unachelewa, bali Neno linakuwa la thamani. Kama tunavyouona, Bwana, wakati baada ya wakati, uwepo unaodumu wa Kristo daima hukutana nasi. Jinsi ninavyokushukuru kwa wema Wako! Jinsi ulivyotuokoa na kuwa ... na kutubariki, jinsi tunavyokushukuru kwa jambo hilo!

Ninaposhika lesa hizi mkononi mwangu, Bwana, ni watu walio na imani, wanaoamini Hili. Jalia kila

pepo, kila ugonjwa uondokee hao watu. Namwamuru kila pepo hapa, aliye mchafu, na asiye wa Mungu, kila pepo wa magonjwa, magonjwa yote na mateso. Sisi hatujilazi katika kivuli cha mwanadamu, ambapo ingekuwa sawa, bali tuko kwenye kivuli cha Injili, Injili iliyothibitishwa.

Huku ile Nguzo kuu ya Moto inapoenenda huku na huko humu jengoni, ile ile ambayo Mungu alitazama moja kwa moja chini, kupitia, nayo Bahari ya Shamu ikaachana, nao Israeli wakapita. Bali sasa, Yeye anapotazama, imenyunyiziwa Damu ya Mwanawe Pekee, ambapo rehema na neema. Hebu tuwe watiifu. Jalia sisi leo tuache kusema, kulilia. Hebu tutambue ya kwamba umetuita kwa ajili ya kazi hii. Hii ndiyo ile saa. Ninanena jambo hilo katika Jina la Yesu Kristo, jalia kila ugonjwa uondokee hapa.

112 Jalia kila mwanamume na mwanamke, anayeliitia Jina la Yesu Kristo, wayatakase maisha yao upya leo. Ninaweka wakfu yangu, Bwana, juu ya madhabahu ya maombi. Najilaza chini, na kujionea haya na kuelekeza kichwa changu ardhini ambako ulinitoa. Bwana Mungu, ninaona aibu udhaifu wangu na kutokuamini kwangu. Nisamehe, kwayo hayo Bwana. Nipe ujasiri. Tupe sote ujasiri.

Ninajisikia, kama Musa, sote tuko njiani tukitoka. Hatutaki kumwacha mmoja. Tunataka kumchukua kila mmoja, Bwana. Wao ni Wako. Ninawadai kwa ajili Yako. Wabariki watu hawa leo, Bwana. Tujalie. Na unibariki, pamoja nao, Baba, na Jina Lako litasifiwa. Utukufu wako utakuwa Wako. Tupe imani hii ya Milele, Bwana, tunapojiweka wakfu Kwako sasa.

113 Mimi, juu ya Biblia hii na juu ya miimbara hii, ninakupa Wewe maisha yangu, Bwana. Ninategemea kila ahadi uliyotoa. Najua ya kwamba zitathibitishwa. Najua ni Kweli. Nipe ujasiri kunena Maneno haya. Nipe ujasiri, Bwana. Nielekeze katika yale nitakayofanya na kusema. Najitolea Kwako, pamoja na kanisa hili, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Imani yangu ... Kwako,
Wewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondoa dhambi zangu zote,
Ee, hebu mimi tangu siku hii
Niwe wako kabisa!

Sasa hebu na tusimame, kwa utulivu sana, tunapouvumisha. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaanza kuvumisha, *Imani Yangu Inakuangalia* — Mh.]

... Kwako,
Wewe Mwana-Kondoo ...

Hebu na tumwinulie tu Yeye mikono yetu sasa.
Ee Mwokozi ...

Jiwekeni wakfu kwa Mungu sasa.
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondoa mashaka yangu yote,
Ee, hebu mimi tangu siku hii
Niwe wako kabisa!

114 Sasa kwa pamoja, huku tumeinua mikono yetu juu. [Kusanyiko linarudia maombi haya, baada ya Ndugu Branham — Mh.] Bwana Yesu, [Bwana Yesu,] mimi sasa [mimi sasa] ninajiweka wakfu Kwako, [ninajiweka wakfu Kwako,] maisha ya utumishi, [maisha ya utumishi,] safi zaidi, [zaidi safi,] imani zaidi, nakulilia, [imani zaidi, nakulilia,] ili niweze kuwa [ili niweze kuwa] mtumishi anayekubalika zaidi [mtumishi anayekubalika zaidi] katika maisha yangu yajayo, [katika maisha yangu yajayo,] kuliko nilivyokuwa [kuliko nilivyokuwa] katika maisha yaliyopita. [katika maisha yaliyopita.] Nisamehe kutokuamini kwangu, [Nisamehe kutokuamini kwangu,] na kuturejeshea [na kuturejeshea] Imani [Imani] waliyokabidhiwa watakatifu mara moja. [waliyokabidhiwa watakatifu mara moja.] Ninajitolea mwenyewe Kwako, [Ninajitolea mwenyewe Kwako,] katika Jina la Yesu Kristo. [katika Jina la Yesu Kristo.]

Sasa tunapoinamisha vichwa vyetu.
Ninapopita katika giza la utata wa maisha,
Na kuzungukwa na huzuni,
Uwe Kiongozi wangu;
Lifukuze giza ligeuke kuwa mchana,
Ondoa hofu zangu zote,
Wala usiniache nipotee
Niende mbali Nawe.

115 Tunapoinamisha vichwa vyetu sasa. Unajisikia kama kwamba Ujumbe wa asubuhi umekufaa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Unakupa ujasiri? ["Amina."] Kama ungefanya hivyo, mwinulie tu Mungu mikono yako, ukisema, "Mungu, ninakushukuru." ["Mungu, nakushukuru."] Niliinua mikono yangu

yote miwili, kwa sababu ninajisikia tu ya kwamba imenisaidia. Imenipa ujasiri.

Baadhi ya mambo niliyosema, sikufikiri nitayasema, bali tayari yamesemwa. Ilikuwa ni karipio kwangu. Nilijikuta mwenyewe nikiwa katika njia sikufikiri nilikuwa hivyo, bali nalijiona mwenyewe nina hatia ya kulia wakati wote, badala ya kunena.

Mungu, nisaidie, tangu saa hii na kuendelea, kwamba nitakuwa mtumishi aliyewekwa wakfu zaidi.

Sijiombei tu mimi pekee. Nawaombea ninyi, pia, ya kwamba, sote, pamoja kama Mwili wa Kristo, tulioitwa tutoke ulimwenguni, tukijitayarisha kuingia kwenye Nchi ya Ahadi, ya kwamba Mungu atanipa ujasiri kunena njia, kuifanya njia wazi kusudi msikose kuzifuatilia hizo nyayo. Nitawaambieni, kwa neema ya Mungu. nitazifuata nyayo Zake zilizojaa damu Yake Yeye aliyenda mbele zetu.

Na msalaba huu uliwekwa wakfu nitaubeba,
Hadi kifo kitakaponiweka huru,
Na kisha niende Nyumbani, nivae taji,
Kuna taji kwa ajili yangu.

Tunakupa hili Wewe, Baba, kuwekwa wakfu kwetu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana Wako. Amina.

[Ndugu fulani anaanza kunena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

116 Tunamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hili. Ishi maisha yaliyowekwa wakfu. Jitoe mwenyewe, kwa utamu, unyenyekevu. Tembea katika Roho. Enendeni, neneneni, vaeni kama Wakristo, wanyenyekevu na wazuri. Msikose hili sasa. Sauti ya Mungu hunena kupitia kwa Neno, inanena kupitia karama. Karama moja inapokuja, nyingine huitangaza, karama nyingine inakuja na kuonesha jambo lilo hilo. Mnaona, hilo linalingana kabisa na Neno na wakati huu pia. Mungu yu pamoja nasi. Jinsi tunavyomshukuru kwa jambo hilo! Sasa kama ninii yetu ...

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kama dada yetu angetupa tuni juu ya:
Peleka Jina la Yesu uendako,
Kama ngao dhidi ya kila mtego;
Na majaribu yanapokuzunguka,
Pumuatu hilo Jina takatifu katika maombi.

Hebu, fanya tu hivyo, nena Neno na unene Jina Lake. Hebu tuimbe sasa tunapo—tunapoachiliwa.
Peleka Jina la Yesu uendako,
Kama ngao ... na ole;
Litakuwa furaha na faraja,
Loo, lipeleke popote uendako.
Jina la thamani ...

Sasa hebu na tupeane mikono, na kusema, "Nitakuombea, ndugu, nawe uniombee."
... Mbinguni;
Jina la thamani, Jina la thamani, Ee ni tamu jinsi gani!
Tumaini la dunia na furaha ...

Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu na tuimbe aya hii inayofuata.
Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao dhidi ya kila mtego;
Majaribu yatakapokuzunguka,
Pumua hilo Jina takatifu katika maombi.
Jina la thamani, Jina la thamani; Loo ni tamu jinsi gani! Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbingu;
Jina la thamani, Ee ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbingu.

117 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, pamoja na mioyo yetu, tukitambua ya kwamba Yesu alisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenituma, yuna Uzima wa Milele wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Tukijua ya kwamba sisi, kwa neema ya Mungu, tunao ndani ya mioyo yetu, tukijitakasa Kwake asubuhi ya leo, kusudi maisha yetu yapate kubadilika, tangu leo na kuendelea, tupate kuwa na mawazo mema. Tutajaribu kuishi vizuri sana na kuwa wanyenyekevu, kwamba, tukiamini yale tunayomwomba Mungu, Mungu atampa kila mmoja. Nasi hatutanena maovu sisi kwa sisi, ama dhidi ya mtu ye yote. Tutawaombea adui zetu na kuwapenda, kuwatendea mema wale wanaotufanyia mabaya. Mungu ndiye Hakimu wa nani aliye wa kweli na wa uongo. Kwa ninii ...

Lakini kwa msimamo huu, na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nitamuuliza rafiki yetu mwema, Ndugu Lee Vayle, kama atafunga mkutano kwa maombi. Ndugu Vayle. Ndugu Vayle.



www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7